ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.

19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.

21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na

	Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.

45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.

65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

BARAZA LA WAWAWAKILISHI

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 9 Juni, 2010

(Mkutano ulianza saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Nakla zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 4 April, 2010.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai kudiriki na kuhudhuria katika mkutano wa ishirini wa kikao cha bajeti cha mwaka 2010/2011, nasema alhamdulillah. Aidha nawaombea wajumbe wenzangu Mwenyezi Mungu awajaalie kheri na mafanikio na wao tumalize mkutano wa ishirini, pia tushiriki mkutano wa kwanza wa kikao cha Serikali mpya.

Mhe. Spika, vile vile nimshukuru Mhe. Rais Amani Abeid Karume kwa ahadi yake ya kupeleka umeme Pemba, " walisema hayawi hayawi sasa yamekuwa. Kwa hivyo nawaomba wananchi wajue kwamba CCM haitanii wala haifanyi dhihaka inalozungumza inafanya kilillahi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa zungumzia suala lako kuhusu Forodhani.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, hoja yangu ni kuwa mwaka jana wakati wa kujadili hotuba ya bajeti wajumbe wawili walitoa hoja hapa na ilikuwa nzuri na tuligemea hapa tutapata majibu mazuri au *appropriation bill*. Kwa sababu wajumbe walitoa hoja kuwa kwa nini hatuna utaratibu wa kuzungumzia namna ya ukusanyaji wa mapato halafu ndio tupange matumizi, hoja ambayo ilianza kutolewa na Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni Mhe. Ali Haji Ali lakini pia ilizungumzwa na Mhe. Muwakilishi wa Mgogoni Mhe. Abubakar Khamis Bakary, kama nilisikia vizuri tuliambiwa katika kikao hiki huenda ikafikiriwa, sasa nilifikiria tutapata ule ili tujue namna gani tunaweza kukusanya pesa zetu kwa sababu mpango sio matumizi na baadae tukae kitako yujue namna gani tunachambua matumizi yetu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe ni kweli kabisa anavyosema Mhe. Haji Mkema Haji, kwamba mkutano wa bajeti iliyopita tulifikia pahala tukaona kwamba kuna jambo kidogo hatwendi vizuri katika suala zima la ukusanyaji wa kodi kwa mujibu wa wakati wa mwaka ule mpya wa fedha yaani kuanzia tarehe 1 Julai, na hili lilikuwa linahitaji kwamba mara baada ya kupitisha bajeti ya serikali basi uwasilishwe mswada wa mabadiliko mbali mbali ya kodi nifanye subira kwa sababu ili *finance bill* ndio inayorekebisha viwango mbali mbali vya kodi, jambo hilo limezingatiwa lakini halijafikia upeo wake vizuri.

Lakini hata hivyo tulifikia makubaliano jana na Mhe. Waziri kwamba aangalie uwezekano wa jambo hili liwasilishwe kama inawezekana mara baada ya kujadili bajeti kuu ya serikali, laa kama hivyo itakuwa hatukuwa kujitayarisha mapema basi angalau mara baada ya kujadili bajeti ya Afisi ya Waziri Kiongozi sisi tukuwemo ndani basi jambo hilo tulitekeleze na amechukua maalekezo hayo na anajitayarisha ili kufanya kazi hiyo. Ilimradi tu Mhe. Rais aweze kutia saini mswada ule ambao unaweza kupitishwa hapa ili uende sambamba tunapoingia kwenye Julei mosi mwaka 2010, basi na wale wanaokusanya kodi hii waweze kutumia sheria hii ili waweze kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria.

Kwa hivyo jambo hilo tumejaribu kujipanga ingawa sasa hivi matayarisho yake hayajawa tayari lakini tutajitahidi ili mambo hayo yaende vizuri kwa mujibu wa taratibu na wakusanyaji wa kodi waweze kukusanya kwa sheria. Nashukuru Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha Mpango wa Maendeleo na Makadiliri ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2010/2011.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 21

Ukasanyaji wa Taka Katika Manispaa ya Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Niliwahi kumsikia mtaalamu mmoja wa Manispaa ya Zanzibar akisema kupitia chombo cha habari akisema kuwa takataka zinazozalishwa kwa siku

ndani ya Manispaa ni tani 200. Maeneo mengine ya nchi yaliyobakia huzalisha tani 150, wakati ambapo uwezo wa kukusanya takataka hizo ni tani 105 sawa na asilimia 30 (30%) tu ya takataka zote kwa siku.

(a) Je, kwa kuwa uwezo wa Manispaa kukusanya takataka hizo ni mdogo, nini itakuwa suluhisho la suala hilo?

(b) Uzoefu wa nchi nyengine unaonyesha kuwa kila nyumba huwekwa mifuko ya aina 3 ya kuwekea takataka: mfuko wa takataka zinazooza, mfuko wa takataka zisizooza na mfuko wa taka za vibati. Kwa nini Zanzibar tunashindwa kuiga jambo hilo zuri?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 21 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa kwa sasa Baraza la Manispaa halina uwezo wa kukusanya taka zote za Mji wa Zanzibar. Ili kuondoa tatizo hilo, serikali kwa kushirikiana na Baraza la Manispaa imefanya mazungumzo na Benki ya Dunia kulisaidia Baraza kiasi cha *USD* 3,000,000 kwa kazi hiyo chini ya mradi mkuu unaosimamiwa na Wizara ya Fedha *(ZUSP)* ambao utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwaka ujao (2011)

(b) Wazo la kuweka mifuko aina tatu kila nyumba ni zuri na Serikali imelipokea, lakini kabla ya kulifanyia kazi linahitaji maandalizi makubwa kwa upande wa Baraza la Manispaa.

- Kwanza utaratibu wa udhibiti wa mifuko ya plastic ambayo inahitajika kwa kweka taka kwa sehemu tatu tofauti.

- Taaluma ya muda mrefu kwa wananchi wetu ili waweze kutenganisha taka hizo.

- Mahitaji ya nyenzo zaidi na vifaa kama magari maalum na sehemu za kutupa taka kitaalamu bila ya kusababisha athari nyengine za kimazingira. Kwa hivyo, kwa sasa ni maperma mno kuanza utaratibu huo wa kutupa taka kama zinavyofanya Nchi za wenzetu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:

a) Kwa kuwa wamekiri kwamba Baraza halijakuwa na uwezo wa kukusanya taka zote lakini soko la samaki la Darajani limekuwa na uchafu mkubwa wa matumbo ya samaki. Je, hata hili watakuwa hawana uwezo wa kusambaza na eneo la kuhifadhi.

b) Taka taka zinaweza kuzalisha nishati mbadala ya umeme. Je, kafika fedha ambazo Benki ya Dunia imetoa imo sehemu ambayo inahusu taka taka zile kukusanywa na kufanyiwa nishati ya umeme.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Suala la usafi wa soko la samaki nakubaliana na wewe kwamba bado haliko katika hali nzuri na katika utekelezaji huo ambao tunaomba msaada kwa Benki ya Dunia marekebisho makubwa yatafanyika ili kuhakikisha uchafu kutokana na samaki na vifaa vyengine unadhibitiwa kikamilifu.

Suala la pili kuhusiana na nishati kutokana na nguvu za taka liwakuwemo pia katika mjadala au msaada ambao tunatazamia kupata kutoka Benki ya Dunia.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Katika Mkoa wa Mjini Magharibi Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kwa nia njema kabisa imeanzisha mpango mzuri wa nyumba kwa nyumba kila siku asubuhi na wananchi wamepewa uzoefu wa kuweka taka zao katika makapu au vipolo ili taka zile zizoleke kwa urahisi, kwa kuwa utaalam huo unatokana na wenyewe baada ya kushauriana vizuri na kwa kuwa mji wetu tuliokuwa nao huu katika Baraza la Manispaa na kuna adha kubwa zaidi za taka na wananchi wanapata usumbufu na mji unakuwa hauna haiba nzuri kuliko Magharibi.
Je, Mhe. Waziri kwa kuwatumia wenzetu wa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi ana mpango gani wa kuhami hili suala ambalo ni zuri la kusafisha nyumba kwa nyumba ili wananchi wazoee na kuondoa kabisa katika mitaa yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Nakubaliana nae *exercise* inayofanywa katika Wilaya ya Magharibi na ambayo inaonekana kupanda kila siku kuhusiana na

umwagaji wa taka au udhibiti wa taka, pamoja na michango ambayo inafanywa ya kukusanya nyumba kwa nyumbwa za wakaazi wa eneo hilo nao wameonesha mashirikiano mema na mazuri lakini kuna wengine bado hawaja na ushirikiano mzuri. Lakini hata hivyo hali ya Wilaya ya Magharibi Manispaa wanahitaji kwenda kujifunza hili tumeliona na linaleta tija katika maeneo ya usafishaji wa taka, suala hili la kwenda kuwapeleka kule kwenda kusoma nasema linaeleweka na baadhi ya sehemu Manispaa wajejaribu kufanya hivyo.

Lakini hapa kitu muhimu ni kupata ushirikiano wa wananchi wa kutoa hizo fedha ambazo zinatakiwa na wateja ambao wanakusanya taka hizo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Katiba jibu lake Mhe. Waziri amekiri kuwa taka zinazokusanyika kila siku ni nyingi kuliko uwezo wake wa kuliondoa na amejaribu kuomba ufadhili kutoka Benki ya Dunia ili kukamilisha tatizo hili.

a) Lakini taka ni taka na zinasababisha maradhi kazaa na maradhi ni hatari, haoni kuwa hali hii iliyokuwepo kwa muda mrefu inaweza kuisababishia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuingia katika kazi ya makusudi ya kutumia fedha nyingi kwa kuokoa maradhi ambayo yanaweza kutokea, kwa sababu ya kutoondolewa hizi taka taka zinazosambaa.

b) Kama Benki ya Dunia hatukubahatika kupata hiyo fedha inayokusudiwa tuseme Mhe. Waziri ana lengo gani alililoliweka kuona kuwa taka taka hizi zinaondoka zote.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Kutokana na hali ngumu ya vifaa na uwezo wa watendaji kazi ndio kulikopelekea Manispaa kwa kupitia Wizara ya fedha kuomba msaada kutoka kwa rafiki zetu Wajerumani, siku zote unapofanya kazi ikakuletea matatizo basi hakuna budi kuomba msaada kwa rafiki zao ili waweze kukusaidia, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba taka zinazozalishwa ni vigumu kwa Manispaa peke yake kuweza kulisafisha jiji letu.

Kwa hivyo Wizara ya Fedha akiwemo msimamizi mkuu wa masuala hayo ndio itaweza kupata mafanikio katika usafishaji wa mji huu na kutokana na hali hiyo tutaweza kuokoa usafi huo uwe wa hali nzuri na kuondosha uchafu ambao kwa muda mrefu unakuwa katika maeneo ya mji huu.

Mhe. Spika, katika utafutaji huu ukishindikana au labda msaada huu ikiwa haujapatikana bado serikali itajaribu kuongezea vifaa manispaa na hasa katika mambo ya magari na usafishaji ili zoezi hili la usafi wa mji wetu lipate kukamilika.

Nam. 53

Fedha za Mishahara ya Walimu Kupitia PBZ

Mhe. Ali Denge Makame - Aliuliza:-

Wizara yako ilitoa agizo kwa walimu wa skuli za mjini kufungua akaunti PBZ na kuchukulia fedha zao za mshahara huko Benki. Lakini kwakuwa PBZ wanaonekana hawakujiandaa vyema kukabiliana na kundi kubwa la wateja, Benki hiyo inaonekana kuzidiwa kuwapatia huduma ipasavyo walimu hao pamoja na wateja wengine.

(a) Mhe. Waziri, ni sababu gani iliyopelekea Wizara yako kuchukua uamuzi huo wa kuwalazimisha walimu kuchukulia mshahara wao benki bila ya ridhaa ya walimu wengi kati ya hao.

(b) Kwa kuwa uamuzi wa kutumia au kutotumia huduma za Benki ni suala la kibinafsi, huoni kwamba Wizara yako haikuwatendea haki walimu hao kwa kuwalazimisha kupokelea fedha zao Benki.

(c) Kwa kuwa walimu wanatumia muda wao mwingi kwenda kufuatilia fedha zao, huoni kuwa ni bora mchakato huo ukasitishwa na kuwabakisha wale ambao kwa hiari yao wanataka kuendelea na huduma hiyo, ili kupunguza usumbufu kwa walimu hao na kuokoa wakati ambao wanauhitaji sana kuwasaidia wanafunzi.

Mhe. Naib Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako Kabla ya kujibu swali Nam. 53 la Mheshimiwa Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilitoa maelekezo kwa Wafanyakazi wake kufunugua akaunti katika Benki ya Watu wa Zanzibar ili waweze kuchukua mishahara yao huko.

Hatua hii inatokana na muongozo wa Wizara ya Fedha na Uchumi uliotaka wafanyakazi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wapokee mishahara yao kupitia PBZ ili:

i) Kuepuka uwezo wa watu waovu kupora mishahara hiyo katika vituo vya ugavi.

ii) Kuepuka wizi wa mishahara unoweza kutokea katika maeneo yanayohifahiwa mishahara hiyo.

iii) Kuepuka mashambulizi yanayoweza kutokea dhidi ya walimu au maofisa wanaochukua mishahara hiyo kutoka Benki kupeleka vituo ni kwa kugaiwa.

iv) Kuhuisha shughuli za benki yetu ya PBZ.

Katika utekelezaji wa zoezi hilo Wizara ya Fedha iliitaka PBZ ianze kutoa huduma hiyo kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuwa ndiyo yenye idadi kubwa ya wafanyakazi na kiwango kikubwa cha fedha za mishahara. Hata hivyo, kabla ya utekelezaji wa zoezi hilo. Wizara ilifanya vikao nauongozi wa PBZ ili kuhakikisha kwamba hapatakuwa na usumbufu wa upatikanaji wa mishahara hiyo.

PBZ waliihakikishia Wizara kwamba wamejiandaa vya kutosha; watafungua vituo vya kutoa huduma na pia kuweka mashine (ATM) za kurahisisha utoaji fedha. Tulikubaliana tuanzie kwa wafanyakazi wa Wilaya ya Mjini tu ili tuone vipiPBZ wanaweza kulifanikisha suala hilo. Hatua nyengine iliyochukuliwa ni kuwaelimisha wafanyakazi kuhusu umuhimu wa kuchukua mishahara yao Benki.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu suala kama ifuatavyo:-

a. Si sahihi kwamba Wizara ililazimisha walimu kufungua akaunti PBZ na kuchukualia fedha zao huko. Lakini walielimishwa juu ya umuhimu wa suala hilo na ndipo walipochukua uamuzi huo. Ni vyema pia ifahamike kwamba hata kabla ya uamuzi huo walimu wengi wanaochukulia mishahara yao PBZ.

Na hata baada ya uamuzi huo wapo walimu katika Wilaya ya Mjini ambao hawachukulii mishahara yao benki hadi leo na wala Wizara haijachukua hatua yeyote dhidi yao.

b. Nakubali kwamba uamuzi wa kutumia au kutotumia huduma za Benki ni suala la mtu binafsi. Lakini kama nilivyoeleza mwanzo Wizara haikulazimisha mwalimu yeyote kupokelea mshahara Benki. Na ndiyo maana hadi hivi sasa Wizara inasambaza mishahara kulipwa walimu ambao bado hawajaamua kupokelea mishahara yao benki.

Kwa hivyo suala la kutendewa au kutotendewa haki halipo.

c. Wizara haina pingamizi kwa mwalimu yeyote asiyetaka kuchukulia fedha zake benki kujiondoa katika utaratibu huo. Hata hivyo, ni vyema tuelewe kwamba kwa wakati huu si busara kuchukua mamilioni ya fedha mkobani na kuzisafirisha huku na kule kwenda kuwalipa wafanyakazi. Tumeshasikia matokeo ya wizi wa fedha za mishahara katika Taasisi mbali mbali za Serikali zikiwemo za Vikosi vyetu vya SMZ.

Hivi sasa inatubidi tutumie polisi wenye silaha kulinda mishahara na wenye mishahara. Askari wetu majukumu mengi na mazito na kwa hivyo kila inapowezekana vyema kuwapunguzia mzigo.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wapokeaji mishara hawa kwenye mabenki haya huwa wanatoka sehemu mbali mbali ya miji yetu na kutumia gharama ya pale kwenye vituoa vya kupokelea ile mishahara.

Je, atanieleza nini kuondosha usumbufu ambao unatokea kukaa muda mrefu wa foleni na kufika siku mbili au tatu hawajapata fedha hiyo na kutumia gharama ya nauli ya kuzifuatilia fedha hizi kwenye mabenki ana utaratibu gani wa kuondosha kadhia hii angalau fedha zile zipatikane kwa wakati na mapema ili wasiondeze hasara zaidi ya kwenda kuzifuata fedha hizi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakubali kwamba mfanyakazi anapokwenda kuchukua mshahara kwa sababu anatoka sehemu mbali mbali za mji wetu ni lazima atumie nauli, na hata kama mshahara huo ukitoka skuli basi ni lazima atumie nauli kwa ajili ya kwenda huko skuli kuchukua mshahara huo.

Suala la utaratibu gani nitachukua Mhe. Spika, Baraza lako lina wajibu wa kuona na kushauri pale ambapo inaona mambo hayaendi vizuri kuishauri taasisi inayohusika kwa kuandaa utaratibu mzuri wa kuweza kufanya hivyo. Tuliposhauri wafanyakazi wetu kupokelea fedha benki tuliona faida nyingi ambazo wafanyakazi wanaweza kuzipata, moja ni pale wanapotaka mikopo mbali mbali kutoka kwenye mabenki yetu, kwa hivyo tulitoa ushauri huu kwa kuzingatia faida ambazo watapata wafanyakazi wetu ambao hivi sasa wengi wao wamekuwa wakidai mikopo hiyo na ili upate mkopo basi ni lazima ufungue akaunti benki.

Kwa maana hiyo Mhe. Spika, utaratibu utategemea na benki yenyewe jinsi ya ufanisi wake kwa hivyo ni wajibu wa baraza hili kuona pale ambapo taasisi haifanya vizuri basi kutoa ushauri na kuelekeza nini kifanyike ili jambo hilo lifanyike vizuri.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kuonegezea tu na kwanza nikiri kwamba kweli katika benki zetu hata katika mwisho wa mwezi kumekuwa na msongamano mkubwa, hii inatokana na kwamba mwamko sasa wa kupokelea mishahara mabenki umekuwepo na tunashukuru sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wao kukamilisha utaratibu wa walimu wao wote kupokelea mishahara benki, sasa benki yetu ya PBZ imeshaandaa mpango wa kutanua matawi zaidi mfano kwa Pemba tunataka kila Wilaya basi kuwe na huruma za benki, tusingependelea walimu watoke Mkoani waje Chake Chake au atoke Makunduchi aje Mjini, sasa tutawafuatilia kule na utaratibu huo tunauandaa kwa kupeleka huduma kule kwenye walimu na kuondosha usumbufu, mipango hiyo ipo njiani na tulizungumza mwaka jana na tutajitahidi kuitekeleza mwaka huu. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 16

Nzi wa Embe

Mhe. Said Ali Mbarouk (Kny: Mhe. Rashid Seif Suleiman) - Aliuliza:-

(a) Kwa kuwa nzi wa embe wanaelekea kuongezeka. Je, Wizara mpaka mwezi huu imeshatumia kiasi gani katika Bajeti ya 2009/2010 katika kupiga vita nzi hao?

(b) Ni lini Wizara italichukulia tatizo hili kama vile Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilivyolichukulia tatizo la Malaria?

(c) Ni asilimia ngapi ya maembe yanayozaliwa yanakumbwa na tatizo hili?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 16 kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika ni kweli tatizo la Nzi wa embe lipo na ni kubwa na limeenea sio Zanzibar tu, hadi Afrika ya Mashariki yote. Tatizo hili limeanza tokea mwaka 1996 baada ya utafiti wa miaka mitatu kukusanya taarifa za wadudu ili kutafuta mbinu za kuwadhibiti hatimaye kazi hiyo ilizaa matunda. Kuanzia mwaka 2006, mbinu za kutumia mitego ambayo ndio njia bora kwa hivi sasa zilianza kwa baadhi ya maeneo na kuonesha mafanikio. Kazi hii ina gharama kubwa kwa vile mitego na dawa zake hununuliwa kutoka nje ya nchi.

Mhe. Spika, kazi ya uwekaji mitego na ufuatiliaji ina gharama kubwa na Wizara imeshatumia kiasi cha shillingi milioni sabini (70,000,000/=) na bado kazi inaendelea.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, tulipokuwa katika kuahirisha moja ya Baraza lako tukufu mwaka jana, Mhe. Waziri Kiongozi aliwashauri wananchi kujishughulisha na kilimo cha embe kama ni zao la biashara.

Na kwa kuwa wananchi wengi hasa Pemba wameitikia wito huo wa kiongozi wao. Kwa kweli hivi sasa miti ya miembe haitoshi kwenye vitalu vya serikali na vya binafsi .

Je, serikali ina mpango gani wa makusudi, kuona kwamba juhudi hizi za wananchi haziathiriwi na funza au nzi wa embe?

Je, katika hili hatuoni kwamba wananchi wetu wataingia hasara na zaidi itapunguza pato la taifa lao?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, ni kweli wananchi wamehamasika katika kilimo hichi cha miembe, tunawaomba waendelee na wasivunjike moyo. Kama nilivyojibu hapo mwanzo kwamba tatizo hili ni la Afrika Mashariki ya Kati nzima. Kwa hivyo serikali inajiandaa

kutafuta fedha kwa wafadhili na pia katika bajeti zetu za serikali kila mara tutakuwa tunaongeza fedha kwa kupambana na wadudu hawa wa embe. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuongezea majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo.

Mhe. Spika, wakati tupo katika *World Economic Forum* pale Dar-es-Salaam, Mhe. Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipata nafasi ya kukutana na Rais wa IFAD. Katika mazungumzo yao moja kubwa walilolizungumza ni suala la wadudu wanaoingia kwenye matunda na yeye kwa moyo mmoja alikubali kutoa fedha kutoka IFAD kulisaidia hili.

Kwa hivyo Wizara ya Kilimo wanalifanyia kazi hilo sasa hivi kuandika mradi na ile *extent* ya tatizo lilivyo na kuli-*submit* IFAD kwa ajili ya kupata wataalamu na fedha ya kufanyia kazi.

Mhe. Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi nitoe maelezo ya ziada ya kumalizia pale dada yangu Mhe. Samia Suluhu Hassan (Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji) alipomalizia. Maelezo yake ni fasaha sana, lakini nimeona nitoe taarifa zaidi ambayo inaweza ikawasaidia waheshimiwa wajumbe.

Namshukuru sana Mhe. Saidi Ali Mbarouk kwa maelezo yake. Ni kweli nilitoa kauli hiyo mwaka jana na ninategemea mwaka huu Mwenyezi Mungu akipenda nitaitoa tena.

Naamini kwa dhati ya moyo wangu kwamba zao hili la embe linaweza kuwasaidia sana watu wenye kipato cha chini ili kuongeza kipato chao zaidi. Kwa maana hiyo nawashukuru wananchi wa Zanzibar kwa kutekeleza ushauri huo kwa vitendo ni jambo ambalo zuri na nawaomba waendelee kufanya hivyo.

Sisi kama serikali, pamoja na hatua hizi ambazo Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji amezieleza. Hatua nyengine tunazozichukua ni kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo moja ni kusambaza kemikali za kuulia nzi hawa. Lakini kama tunavyojua dawa hizi zinatoka nje na gharama yake ni kubwa sana. Kwa hivyo hatujaweza kuisambaza kiasi cha kutosha. Tatizo hili linaonekana ni kubwa sana.

Hivi karibuni serikali kwa kupitia Wizara ya Kilimo tumepata taarifa ya kutupa faraja sana. Wapo wakulima wa Zanzibari wazalendo mamegundua

dawa ya kuulia nzi hawa wa matunda, wanachanganya kungu manga pamoja na karafuu. Tukadhani kwamba jambo hili ni zuri. Sasa kwa kupitia Wizara ya Kilimo tumewashauri wakae na wakulima ikiwezekana tuwasaidie fedha ili waongeze uwezo wao na utaalamu ili dawa hii iweze kuzalishwa kwa wingi zaidi na iweze kusambazwa kwa wakulima wengi zaidi. Jambo hili likifanikiwa basi naamini tutaleta mapinduzi makubwa katika kilimo hichi cha maembe na matunda kwa ujumla. Kwa hivyo, nawahakikishia waheshimiwa wajumbe kwamba tutafanya kila lililo katika uwezo wetu kutekeleza agizo hilo na dhamira hiyo njema.

La tatu ambalo ni muhimu sana, kama tunavyojua siku hizi kumekuwa na uingizaji mkubwa sana wa matunda kutoka nje ya Zanzibar, yapo yanayotoka Mombasa, Tanzania Bara. Katika maeneo haya zipo taarifa kwamba katika ukanda wetu huu wa Afrika Mashariki hawa nzi wa matunda wameenea. Kwa maana hiyo sisi kama serikali tunatakiwa kujiimarisha zaidi ili kuhakisha matunda haya yanayoingizwa kutoka nje ya Zanzibar yanazibitiwa. Kwa sababu hata tukifika mahali tukifanikiwa kupata hiyo dawa na tukaweza kuwatokomesha hao wadudu. Kama tatizo hilo lipo la kuchukua matunda kwenye sehemu nyengine na yanaingizwa tu bila ya utaratibu.

Mhe. Spika, mimi nadhani kila wakati tatizo hilo litakuwa linajirudia rudia, lakini mimi naomba kama nilivyosema sisi kama serikali tutafanya kila lililokuwepo katika uwezo wetu ili kulisimamia jambo hilo ili wakulima wetu waweze kupata fursa ya kujiendeleza kimaisha. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii, naomba niulize swali moja la nyongeza. Nilipokuwa nikisoma skuli nilifundishwa hesabu za maji yanayoingia katika pipa, huku yanaingia huku yanatoka. Kwa hiyo nataka nizitumie hesabu hizo kuuliza swali langu.

Mhe. Spika, kama Wizara ya Kilimo imeshafanya utafiti wa kujua nzi wanaongezeka kwa asilimia ngapi kwa mwezi katika visiwa hivi. Naomba kujua

Je, wameshafanya utafiti huo kuweza kujua ni asilimia ngapi zinazoongezeka kwa mwezi na asilimia ngapi wanaokufa kwa mwezi, kutokana na dawa zetu tunazowaingizia ili tukajua ni asilimia ngapi ya ongezeko au ya punguzo la nzi wanaoingia?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi hii kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mula baada ya

majibu mazuri ya Mhe. Waziri Kiongozi na Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji na Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo.

Kwa kweli zoezi hili sisi hatujalifanya, lakini napenda kukuhakikishia kwamba dastruri yetu tutalijibu kwa maandishi na ikiwezekana kabla ya kikao hiki kumalizika tutakupatia.

Nam. 2

Kuongezeka kwa Maradhi ya Ukoma:

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Mhe. Waziri, kwa nini pamoja na jitihada zinazochukuliwa na serikali kupitia Wizara ya Afya ikiwemo utoaji wa elimu kwa jamii ili kupiga vita maradhi ya ukoma, bado maradhi hayo yanaongezeka.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika si sahihi kusema kuwa ugonjwa wa Ukoma umeengezeka hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Ugonjwa wa Ukoma hauongezeki hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Katika mwaka 2000 hadi 2007, Zanzibar tumekuwa tukigundua wastani wa wagonjwa wapya wa Ukoma wapatao mia moja (100) kwa kila mwaka.

Katika utafiti wa mwaka 2005 *(active case finding)* jumla ya wagonjwa wapya wa Ukoma 125 waligunduliwa. Idadi ambayo ni zaidi ya wagonjwa wanaopatikana kwa mwaka kwa njia ya kawaida *(passive case finding)* yaani wenyewe katika vituo vya Afya na kugunduliwa Ukoma.

Kuanzia mwaka 2008- 2009 pamoja na jitihada nyengine za utafiti *(active case finding*) inaonekana kuwa idadi ya wagonjwa wapya wa ukoma kwa mwaka imepungua hadi kufikia wagonjwa 65.

Kwa hivi sasa Zanzibar tuna wagonjwa wa Ukoma 1.2 kwa kila watu elfu kumi ambapo lengo l;a kimataifa *(WHO)* la kutokomeza ugonjwa wa Ukoma ni kuwa na mgonjwa si zaidi ya mmoja kwa kila elfu kumi.

Suala ambalo wizara yangu kupitia kitengo cha kifua Kikuu na Ukoma inaendelea nalo, na kutoa elimu ya afya kwa jamii kwani ndio njia kuu ya kuwatanabahisha wananchi kujitokeza mapema kuchunguzwa mabaka ili ukoma ugunduliwa mapema kabla haujaleta athari za Ulemavu.

Mhe. Spika , napenda kutoa wito kwa wajumbe wote wa baraza lako tukufu kuwa suala hili la Ukoma tuwakumbushe wananchi ili waitikie wito kwa sababu dalili za awali za ugonjwa wa Ukoma ni baka au mabaka katika ngozi na mabaka ya Ukoma hayawashi wala hayaumi na yana rangi kama ya shaba.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Zanzibar kupitia kitengo cha Kifua Kikuu na Ukoma Zanzibara tayari tumeandaa mikakati ya kutokomeza ugonjwa wa Ukoma kwa kushirikiana na wadau mbali ikiwa pamoja na Shirika la Afya Duniani *(WHO)*.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii kuweza kumuuliza swali Mhe. Waziri.

Zamani hawa watu waliokuwa na maradhi haya walikuwa wanakaa peke yao, wanakuwa mbali kabisa na watu waliokuwa hawajaugua haya maradhi, sasa hivi wapo karibu. Nafikiri hili ongezeko pengine linatokana na hii kuwa na ukaribu.

Je, ana mpango gani wa kinga kwa wale waiozunguukwa na mazingira haya kwa wale waliokuwa hawajapatwa na haya maradhi.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, ni kweli na ni sahihi zamani wagonjwa wa ukoma walikuwa wanatengwa hapa Zanzibar walikuwa wanawekwa Welezo na Pemba walikuwa wanawekwa Makondeni. Hivi sasa jamii hatufanyi kuitenga bali tunataka wajitokeze wenyewe wagonjwa au wanapokwenda hospitali tunawapa dawa za MMDT dawa za mchanganyiko. Dawa hizi mgonjwa akipewa tu hakuna athari yoyote na anakuwa hana uwezo tena wa kuambukiza.

Wito wetu ni kwamba yeyote anayejihisi na mabaka katika mwili wake ajitokeze haraka ili tuweze kumpatia dawa hizi. Dawa hizi zipo kwenye vituo vyote vya afya kwa Unguja na Pemba na zinapatikana bure bila ya malipo yoyote. Kweli ni sahihi kuwa maradhi haya ni mabaya kwa sababu yanaambulikiza kwa njia ya hewa si maradhi mazuri ni maradhi thakili kabisa.
Wito wangu kwa mara nyengine tena naomba wananchi wote wanaonisikia mwenye baka la aina yoyote anayekuwa na wasi wasi haraka aende kituo cha afya ili akatibiwe.

Mhe. Subeti Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri, zamani serikali ilikuwa na utaratibu wa kuwasaidia wagonjwa hawa wa ukoma kwa kuwafariji, kuwasaidia kula, nyumba na dawa. Je, utaratibu huu bado unaendelea au umekufa. Kama umekufa hatuoni kama ule utaratibu wa kuwasaidia ulikuwa na mzuri na ni wakuwafariji ndugu zetu.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, ni sahihi Mhe. Mwakilishi anayaelewa zaidi haya maradhi inaonekana. Zamani tuliwawekea mpaka sehemu ya kuishi huko Pemba lakini hivi sasa tunachokifanya wale wagonjwa wote ambao wameathirika kwa njia ya ulemavu hao huwa tunawapitia, tunawapa elimu ya *safe care*, namna ya kujiangalia wenyewe, na wenye matatizo tunawafanyia *operation* kwa kuwaweka sawa. Na wale wenye matatizo makubwa tunawapeleka Tanzania Bara katika Mkoa wa Shinyanga unaoitwa Kolandoto kwa kufanyiwa *operation*. Wagonjwa walioathirika kwa njia ya ulemavu huwa tunawafatilia na tunawaangalia na kuhakikisha kwamba mambo yao yote yanakuwa mazuri na hayana matatizo yoyote.

Mhe. Abubakar Khamis Bakari: Mhe. Spika, na mimi naomba niulize swali moja. Swali alilouliza Mhe. Subeti lilikuwa ni suala la *maintenance* kwa chakula kwa fedha na kwa mambo kama hayo.

Mhe. Waziri naona kama hajalijibu. Je, wale wagonjwa kwa mfano waliokuwepo Makundeni katika jimbo langu hawapewi chochote na serikali ni wawakilishi na wabunge na watu wenye usamaria mwema ndio wanaowalisha? Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia watu kama hawa?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, ni sahihi kwa hivi sasa hatuna uwezo wa kuwasaidia chakula na fedha kwa kila mgonjwa aliyepata na ulemavu wa maradhi haya.

Mhe. Spika, lazima nifahamishe kwamba wale wanaougua ukoma tukiwatibu mapema hawapati ulemavu. Wale waliochelewa, waliokaa muda mrefu, kwani maradhi haya ukiyapata Mwenyezi Mungu atuepushe na ukachelewa kupata matibabu unapata athari za kukosa hisia za *nerves* kwa hivyo matokeo yake unapata ulemavu. Sasa suala la kuwasaidia hawa kwa njia ya chakula na fedha hilo bado, lakini serikali tutaliangalia namna ya kuwahudumia.

Makundeni Pemba, kama ninavyofahamu miye na nimeshatembelea sehemu ile wamepatiwa sehemu ya nyumba, wenyewe utawakuta wanalima na wanajiendeleza maisha yao vizuri. Wakati mmoja waliomba wapatiwe hati miliki ya eneo lile liwe mali yao. Ombi hili nilipewa lakini bado tunalishuhulikia serikali.

Kuhusu kupatiwa chakula na fedha hawa wazee nafikiri Mhe. Spika, tumelipokea hili suala na tutaliangalia uzito wake.

Nam. 12

Udhibiti wa Magari ya Serikali

Mhe. Haji Mkema Haji - Aliuliza:-

Katika Kikao cha Bajeti cha 2009/2010 Wajumbe wa Baraza hili tukufu walio wengi waliilalamikia matumizi mabaya ya magari ya serikali na walishauri kuwa magari yote ya serikali yatengenezwa kwenye Karakana za Serikali.

(a) Je, Mhe. Waziri, ushauri huo umetekelezwa kwa kwa kiasi gani?

(b) Magari ya serikali kutembea baada ya saa za kazi na siku za siku kuu imekuwa ni jambo la kawaida. Je, serikali imehalalisha utaratibu huo au imeshindwa kudhibiti magari yake?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-
Mhe. Spika awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria katika Kikao cha Baraza na kuweza kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi jibu lake nambari 12 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na ushauri wa Mhe. Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba magari ya serikali yatengenezwe kwenye Karakana za Serikali lakini utekelezaji wa ushauri huu unategemea uamuzi wa Wakuu Taasisi husika za serikali. Hata hivyo hadi sasa mbali na gari ya wizara yangu ni gari chache za serikali ambazo zinapelekwa Karakana Kuu, gari hizo ni za Bodi ya Mapato (ZRB), Chuo Kikuu ca Taifa (SUZA), Wizara ya Fedha na Uchumi, Mkoa wa Mjini/ Magharibi na gari za Shirika la Umeme.

(b) Kuhusiana na magari ya serikali kutembea baada ya saa za kazi na siku za sikuuu, serikali haijahalalisha utaratibu huo kwani katika kifungu cha 25 cha sheria nambari 13 ya mwaka 2004 inayohusiana na udhibiti wa magari ya serikali inakataza magari ya serikali kutembea bila ya kibali maalum baada ya saa za kazi au siku za sikuu isipokuwa kwa magari yafuatayo:-

(i) Magari ya serikali yanayomilikiwa na Vikosi vya SMZ;

(ii) Magari yanayotumika kwa ajili ya kubeba wagonjwa na shughuli za Zimamoto;

(iii) Magari ya serikali yanayotumiwa na Wateuliwa wa Rais; na

(iv) Magari ya serikali yanayotumiwa na Viongozi Wakuu wastaafu wa serikali, Spika, na Kiongozi wa upinzani wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Mawasiliano na Uchukuzi naomba kuuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, tunajua dhamana ya magari ya serikali imepewa wizara hii ya Mawasiliano. Sasa mheshimiwa akisema kuwa magari yanapelekwa huku kwa kutegemea wakuu wa taasisi si kukwepa dhamana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwa sababu ya ushauri alioutoa Mhe. Mwakilishi wizara yangu itashirikiana na Afisi ya Waziri Kiongozi kuona kwamba utekelezaji wa sheria hii unafuatwa kama ulivyoagizwa.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, ahsante sana nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika jibu lake mama amesema kwamba haya yanategemea na uwamuzi wa taasisi husika maana taasisi ikiamua tu kwamba tusende huku tunakwenda huku hivyo ndivyo alivyojibu yeye.

Sasa mimi namuuliza haoni kwamba maamuzi hayo yanatokana na kuwa na ukosefu mkubwa wa vifaa katika karakana yake. Na je, wana mpango gani wa

kuona kwamba hii karakana inaimarishwa ili hizo taasisi zisiweze kuchukua uwamuzi wanaopenda wao.

Mhe. Spika, kwa sababu kuna gereji moja ya bwana mmoja anaitwa Juma Buda nafikiri serikali hawaifikii kwa vifaa vyake. Sasa wana mpango gani wa kuona kwamba karakana ya serikali inakuwa na vifaa na kila kitu ambacho kitafanya iwe hakuna sababu ya mtu katika taasisi ya serikali kutoa uwamuzi wa kwenda pahali pengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza pamoja na Mhe. Zakia kuuliza swali lakini pia ametushauri kwa upande wa serikali. Kwa hivyo kwanza nataka nimjibu kwamba ushauri wake tumeupokea. Lakini vile vile mbali ya kuwa na suala la vifaa pia mafundi nao wanatakiwa sasa hivi waende na teknolojia za sasa kwa sababu magari yaliyotengenezwa zamani na hivi sasa yanautofauti huo. Kwa hivyo hilo nalo pia tutalifanyia kazi kuona kwamba tatizo hilo linaondoka kupitia utaratibu ambao tumeuzungumza.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nimuulize Mhe. Waziri suala la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kwa kuwa wamekiri kwamba baadhi ya taasisi wanakwepa agizo hili la serikali. Na kwa kuwa Baraza mara zote hupitisha kifungu cha matengenezo ya magari ya serikali.

(a) Je, atakubaliana na miye kwamba kifungu hichi cha matengenezo ya magari ya serikali hakitumiki vyema?

(b) Kwa kuwa kifungu hiki hakitumiki vyema bajeti tushauri kwamba taasisi ambazo wanakwepa jukumu hili tusiwatilie pesa?

Mhe. Waziri wa Nchi Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze kwa ushindi wa kishindo kwenye kura za maoni (*Makofi*).

Mhe. Spika, kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri kwamba kutokana pengine na kutokuwa na vifaa vya kutosha wizara yangu mwaka jana ilizungumza kwamba tulitoa fursa kwa taasisi nyengine za serikali kama Karakana ya Matrekta, Chuo cha Karume Mbweni kutusaidia kazi hii kwa muda hadi karakana ile itakapokuwa na uwezo wa kutosha. Kwa hivyo bado tunaruhusu na sehemu hizo nazo kutengeneza gari za serikali.

Kuhusu kuzuia mafungu hili nafikiri ni wajibu wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuangalia wizara kwa wizara kwa sababu mafungu yote ya

wizara anawajibika Katibu Mkuu wa Wizara husika, sasa akipeleka nje ya huko Katibu Mkuu mwenyewe ndiye atakuwa na jibu la kusema kwa wizara husika sio Wizara ya Mawasiliano izuiliwe mafungu.

Mhe. Spika: Maswali yamemalizika yalipangwa kwa leo. Shughuli inayofuatia hiyo itafanywa jioni. Kwa hivyo sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kutoa hoja ya kutenga kanuni kando ya baadhi ya kanuni ili Baraza lako tukufu liweze kutekeleza majukumu yake kwa urahisi na kwa ufanisi zaidi katika mkutano wetu huu wa 20. Utakaojadili na kupitisha bajeti ya serikali kwa maka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, naliomba baraza lako tukufu likubali kutenga kanuni kando zifuatazo:-

1) Kanuni ya 24(1) inayohusu nyakati za vikao. Naliomba Baraza likubali kwamba leo tarehe 9/6/2010 kikao chetu cha jioni kianze saa 10 badala ya saa 11.

2) Naliomba Baraza lako tukufu likubali kwamba katika mkutano huu kuanzia wiki ijayo vikao vya Baraza viwe vinafanyika hata siku za Jumamosi.

3) Kanuni ya 94(3) inayohusu kiwango cha muda wa mawaziri kuwasilisha hotuba za makadirio ya wizara katika mkutano huu wa 20, tunapendekeza kila waziri atumie muda usiozidi dakika 45 kuwasilisha muhtasari wa hotuba yake. Isipokuwa uwasilishwaji wa Bajeti ya Serikali na Bajeti ya Waziri Kiongozi utatumia muda wa kawaida.

4) Kanuni ya 58(6) inayohusu muda anaopewa mjumbe wa kuchangia hoja tunapendekeza katika mkutano huu mjumbe apewe muda wa dakika 15 mpaka 20.

5) Tunaliomba Baraza likubali kwamba muda wa hotuba za wenyeviti wa Kamati na muda wa hotuba za mawaziri vivuzi usizidi dakika 30. (*Vicheko*)

Mhe. Spika, naomba radhi na naomba kurejea.

Tunaliomba Baraza lako tukufu likubali kwamba muda wa hotuba za wenye viti wa Kamati na muda wa hotuba za mawaziri vivuli usizidi dakika 30.

Mhe. Spika: Huo ni utelezi wa ulimi, tunamsamehe. Endelea

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi:

6) Mwisho tunaliomba Baraza lako tukufu kutoa muda usiozidi saa moja kwa waziri husika kwa ajili ya ufanyaji majumuisho ya kujibu hoja za wajumbe katika Bajeti ya kila wizara.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi, nadhani tukiri tu kwamba nyama hii iliyo kinywani ikiteleza inaweza yakapatikana matatizo makubwa kama yalivyomfika Mhe. Waziri. Kiubinaadamu na udhaifu wa binaadamu basi tunamsamehe kwa kweli umetupeleka mahali ambako siko.

Waheshimiwa wajumbe basi niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi, wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa wajumbe nakushukuruni kwa mashirikiano makubwa tuliyoanza asubuhi hii ya leo kwa kipindi hichi cha masuali. Sasa niahirishe kikao hiki hadi saa 10 jioni kusikiliza hotuba ya bajeti. Ahsante sana.

(Saa 4:04 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA

WA FEDHA 2010/2011

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati Maalum ili liweze kupokea Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, nawasilisha mbele ya Baraza lako tukufu na wananchi wa Zanzibar mapendekezo haya nikitimiza matakwa ya kifungu cha 105 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kama ilivyorekebishwa na kifungu cha 17 cha Sheria ya Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2005.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kuwasilisha kwa muhtasari tu mapendekezo haya ambayo yanapaswa kusomwa pamoja na vitabu vitatu vinavyoeleza na kubainisha kwa kina Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Kitabu cha kwanza kinahusu Mapitio ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2009/10, kitabu cha pili kinaelezea Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na kupendekeza Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2010/2011 na kitabu cha tatu ni Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2010/2011. Naomba maafisa wa "*Hansard*" waweke kwenye kumbukumbu yote yaliomo kwenye vitabu vyote vitatu. Waheshimiwa Wajumbe wanaombwa pia wajadili na hatimae kuidhinisha utekelezaji wa mapendekezo haya.

Mhe. Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenye ukarimu aliyetujaalia uzima wa afya na amani katika nchi yetu na akatuwezesha kukutana tena kuyajadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Aidha, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa pamoja leo hii wajumbe wa vyama viwili tukiwa wenye furaha na utulivu mbele ya Baraza hili tukufu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie umoja, mshikamano, hekima na busara katika kujadili, kushauriana na hatimae kuupitisha Mpango wetu wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2010/11 ili tuweze kufikia malengo tuliyoyakusudia.

Mhe. Spika, naomba kutumia fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati, kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Uchumi, kwako wewe binafsi kwa kuliongoza vyema Baraza hili tukufu. Shukrani zetu zinakwenda pia kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza hili tukufu, Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza lako, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Baraza hili na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza kwa mashirikiano, maoni na muongozo wao katika kipindi chote cha mwaka unaoendelea wa fedha na katika maandalizi ya bajeti

hii ninayoiwasilisha mbele yenu. Ushauri, mapendekezo na maelekezo yao waliyokuwa wakiyatoa kupitia kamati na vikao mbali mbali kwa kila wizara yamesaidia kwa kiwango kikubwa kuikamilisha bajeti hii.

Mhe. Spika, katika mwaka huu wa fedha Baraza letu limeshuhudia kukua kwa demokrasia na kuvumiliana kisiasa. Maendeleo hayo muhimu kwa jamii yetu yamepelekea kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kuwateua Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kutoka Chama kikuu cha upinzani, CUF, kuwa Wajumbe wa Baraza hili. Naomba pia kutoa pongezi maalum kwa Mhe. Thuwayba Edington Kissassi kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza kufuatia kupitishwa kwa Kanuni mpya inayozingatia jinsia katika uongozi wa Baraza. Safu ya uongozi wa Baraza letu sasa imekamilika kwa kuhusisha jinsia zote mbili.

Mhe. Spika, ninawajibu mkubwa wa kutoa shukrani zangu za dhati na za kipekee kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Amani Abeid Karume kwa uongozi wake wa hekima na busara katika kuiongoza nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza pia Mhe. Rais kwa bidii na jitihada zake binafsi za kuiletea nchi yetu utulivu wa kisiasa na kijamii kupitia maridhiano baina ya vyama na watu wote wa Pemba na Unguja. Namuomba Mwenyezi Mungu, ampe nguvu na uwezo wa kulikamilisha zoezi hilo kwa manufaa ya Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Mhe. Spika, pongezi pia zinakwenda kwa Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad, Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), kwa mchango wake katika siku za hivi karibuni katika juhudi za kuleta utulivu na umoja nchini mwetu. Ni imani yangu kuwa Wazanzibari sote wenye sifa tutaitumia vyema fursa ya kura ya maoni hapo tarehe 31 Julai, 2010 kuchagua mfumo wa Serikali tunaouafiki kwa mustakabali mwema wa nchi yetu na vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena Wizara ya Fedha na Uchumi imeendelea kufaidika sana na hekima na busara za Mhe. Rais katika utekelezaji wa majukumu yake. Naomba nitumie fursa hii adhimu kumshukuru kwa dhati kwa uongozi, dira na busara zake zilizowezesha mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika utekelezaji wa majukumu ya serikali kuu kwa ujumla na wizara ya Fedha na Uchumi kipekee.

Mhe. Spika, upeo wa uongozi na utulivu wa Mhe. Dk. Amani Abeid Karume umesaidia sana kuivusha salama na kwa mafanikio nchi yetu wakati dunia ilipokumbwa na misukosuko ya kupanda kwa bei za mafuta, chakula na misukosuko ya fedha baina ya miaka ya 2007 na 2009. Busara zake pia

zilionekana wakati kisiwa cha Unguja kilipokumbwa na mtihani wa kukosa umeme kwa kipindi cha miezi mitatu baina ya Disemba 2009 hadi Machi 2010.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii, kuungana na Mhe. Rais na viongozi wengine wa Serikali waliowashukuru kwa dhati Wazanzibari na wageni wetu wote kwa utulivu wao katika vipindi hivi viwili vigumu. Kwa mara nyengine tena, Wazanzibari tumeonesha dunia kiwango cha juu cha uelewa, ustahamilivu, na uungaji mkono kwa viongozi wetu pale nchi inapokumbwa na mitihani mbali mbali. Tunawashukuru sana. Hapo baadae nitaeleza kwa undani hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na tatizo hilo na kuepusha lisitokee tena nchini mwetu.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/10 Serikali ilipanga kutekeleza bajeti iliyoitwa "Bajeti ya Miundombinu kwa kuimarisha Kilimo na Utalii" sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020, malengo ya MKUZA yaliyozingatia Malengo ya Milenia (*MDGs*) pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005.

Kipindi hicho cha utekelezaji kimeshuhudia pia kufanyika kwa mapitio ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya MKUZA yaliyopelekea kufanyika kwa tafiti mbali mbali zilizoibuwa hoja zinazosaidia katika matayarisho ya awamu ya pili ya MKUZA. Mkakati wa Mageuzi ya Utumishi Serikalini nao umeendelea kutayarishwa kwa kuhusisha pia mageuzi ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, hotuba yangu hii itawasilisha muhtasari wa tathmini ya utekelezaji wa Mwelekeo wa Sera za CCM kwa miaka 2000 – 2010, Mapitio ya Hali ya Uchumi Duniani, Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2009/10 na Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa 2009/10. Hotuba pia itazungumzia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2010/11 na kugusia hatua za utayarishaji wa awamu ya pili ya MKUZA (MKUZA II).

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MWELEKEO WA SERA ZA CHAMA TAWALA (CCM) KWA MIAKA YA 2000-2010

Mhe. Spika, kila baada ya miaka 10, CCM hutoa "mwelekeo" ambao ni dira inayoongoza kwa kipindi cha miaka 10. Kwa kuwa CCM ndio chama tawala, dira hiyo pia ndio inayoongoza Serikali zake katika kuimarisha majukumu yake, pamoja na kupanga malengo na mikakati ya utekelezaji wake. Ilani za Uchaguzi za CCM ya mwaka 2000-2005 na 2005-2010 ziliandaliwa kutokana na mwelekeo huo. Malengo makuu ya mwelekeo wa sera za CCM kwa

mwaka wa 2000-2010 ni kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea na uwezeshaji wa kiuchumi kwa wananchi.

Tathmini ya jumla

Mhe. Spika, ili kutekeleza sera za CCM kwa kipindi cha miaka 2000–2010 SMZ iliandaa Dira ya 2020 ambayo utekelezaji wake umejumuisha uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Awali wa Kupunguza Umasikini Zanzibar (*ZPRP*) uliotekelezwa miaka ya 2002/03–2005/06 na utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA) 2007-2010 pamoja na utekelezaji wa sera mbali mbali za kisekta kwa kipindi hicho. Serikali pia iliandaa na kutekeleza sera za mageuzi ya kiuchumi na fedha, kitaasisi na watendakazi na utawala bora ambayo yameongeza ari na kasi ya ukuaji wa uchumi, usimamizi mzuri wa mapato, udhibiti mzuri wa matumizi ya Serikali na kuweka mazingira bora ya utendaji wa kazi kwa taasisi za Serikali.

Mhe. Spika, katika miaka ya awali ya kipindi cha miaka ya 2000–2010 tumeshuhudia, kufanyika kwa jitihada za makusudi zilizolenga kurejesha imani ya Washirika wa Maendeleo na hivyo kuongeza mashirikiano yao na Serikali na Watu wa Zanzibar. Uimarishaji wa demokrasia, usimamizi bora wa uchumi, na azma ya Serikali ya kuimarisha amani, utulivu na usalama nchini, ni mambo yaliokuza imani ya Washirika wa Maendeleo na hivyo kwa kiasi kikubwa kuanza kuziunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuwaletea wananchi wake maendeleo endelevu.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki cha miaka 10 ya utekelezaji wa Sera za CCM nchi ilishuhudia matokeo mengi ndani na nje ya nchi ambayo yaliathiri maeneo mengi ya uzalishaji na utoaji huduma. Mwanzoni mwaka 2000 matokeo ya kigaidi kama vile mashambulizi ya Septemba 11, 2001 huko Marekani; 11 Machi 2004 Madrid Spain na Julai 7, 2005 Uingereza, yaliathiri uchumi duniani ikiwemo Zanzibar. Katika nusu ya pili ya utekelezaji, dunia ilikumbwa na misukosuko ya chakula, mafuta na fedha na kusababisha athari katika ukuaji wa uchumi na mfumko wa bei na kuathiri hali ya maisha ya wananchi wa kawaida. Nchi yetu pia ilishuhudia kufikwa na tatizo la kukatika kwa umeme mara mbili ambalo liliathiri uzalishaji na utoaji wa huduma muhimu katika maeneo mengi nchini mwetu.

Mhe. Spika, pamoja na matatizo ya nje na ndani tuliyoyapata, juhudi za Serikali, viongozi na wananchi kwa jumla zimewezesha kukabiliana nayo vyema na hatimae kuweza kupata mafanikio mazuri katika uchumi kuliko tulivyotarajia kutokana na misukosuko hiyo. Mafanikio katika utekelezaji wa

baadhi ya sekta kwa kipindi cha utekelezaji wa mwelekeo wa sera za CCM za 2000 mpaka 2010 ni kama ifuatavyo:-

Utekelezaji Halisi wa Mwelekeo wa Sera za CCM za 2000 - 2010

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka 2000-2010 uchumi wa Zanzibar uliendelea kuimarika zaidi. Ukuaji halisi wa pato la Taifa kwa Zanzibar kati ya mwaka 2000 hadi 2009 ni wastani wa asilimia 6.8 kwa mwaka. Ukuaji ulifikia asilimia 6.7 mwaka 2009 kutoka asilimia 3.6 mwaka 2000. Pato halisi la Taifa limeongezeka kwa asilimia 38.9 kati ya mwaka 2000 hadi 2009. Wastani wa Pato la Kila Mtu kwa bei za miaka husika (*current prices*) limeongezeka hadi kufikia Tsh. 728,361 (USD 557) mwishoni mwa mwaka 2009 kutoka Tsh. 207,987 (USD 260) mwaka 2000.

Mhe. Spika, licha ya mwenendo wa kuridhisha wa ukuaji wa pato la Taifa, mfumko wa bei ndani ya kipindi cha utekelezaji wa mwelekeo wa sera za CCM kwa kipindi cha 2000-2010 imekuwa ni changamoto kwa maendeleo ya watu. Katika kipindi cha mapitio, mfumko wa bei umekuwa ukiongezeka japo kwa viwango vinavyotofautiana. Sababu kuu zilizopelekea mfumko huo wa bei ni pamoja na hizi zifuatazo:-

1. Uzalishaji mdogo wa chakula usiokidhi mahitaji ya nchi na kuchangiwa pia na kupanda kwa bei za vyakula duniani;

2. Athari ya kupanda mara kawa mara kwa bei ya bidhaa za petroli duniani;

3. Msukosuko wa fedha/uchumi wa dunia uliotokea kuanzia mwaka 2008; na

4. Ujenzi wa Bandari ya Malindi uliozorotesha uingizaji wa bidhaa mbali mbali kutoka nje kwa mwaka 2008.

Hali hii ilipelekea bidhaa zenye thamani ya Tsh 93,439 milioni tu kuingizwa nchini ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya Tsh 107,689 milioni zilizoingizwa mwaka 2007. Mfumko wa bei umeongezeka kutoka asilimia 5.1 mwaka 2000 hadi asilimia 9.7 mwaka 2005. Mwaka 2008 uliweka rekodi kwa mfumko wa bei kuendelea kupanda na kufikia asilimia 20.6 kutokana na mchanganyiko wa sababu zote tatu zilizioelezwa hapo awali. Kipindi hicho kilishuhudia kiwango cha juu cha bei za bidhaa za petroli, mchele, unga wa ngano na sukari. Habari njema ni kuwa mwaka 2009, kasi hiyo imepungua na kufikia asilimia 8.9 kufuatia kushuka kwa bei za vyakula na mafuta duniani kwa wakati huo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mapitio haya, kasi ya ukuzaji wa raslimali imeonesha kuongezeka mwaka hadi mwaka kutoka thamani ya Tsh 24,445 milioni mwaka 2000 hadi Tsh 175,877 milioni mwaka 2009. Uwiano wa ukuzaji wa rasilimali kwa Pato la Taifa umepanda kutoka kiwango cha asilimia 12.8 mwaka 2000 hadi asilimia 20.1 mwaka 2009. Takwimu zinaonesha kuwa ukuzaji rasilimali mkubwa ulifanyika katika vyombo vya usafiri, ujenzi wa nyumba za kuishi, na ujenzi wa miundo mbinu ya barabara, uendelezaji wa ardhi, na utalii.

Mhe. Spika, usimamizi mzuri wa fedha za umma ni moja ya eneo muhimu la utawala bora. Serikali imechukua hatua za kuimarisha taratibu za Bajeti na uandaaji wa mipango ili iende sambamba na utekelezaji wa malengo ya kitaifa na kimataifa na kuweka ukadiriaji bora wa mapato na usimamizi mzuri wa matumizi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka kumi ya 2000-2010 baadhi ya hatua zilizochukuliwa kuimarisha taratibu za mipango na bajeti ni hizi zifuatazo:

i) Kupanua wigo wa kodi, kuimarisha mfumo wa sheria za usimamizi wa kodi/mapato, na kuziimarisha taasisi za usimamizi wa mapato *(TRA & ZRB);*

ii) Maandalizi ya mipango mikakati ya kila Wizara;

iii) Uanzishaji wa utaratibu wa *MTEF*;

iv) Uanzishaji wa utaratibu wa kufanya tathmini ya matumizi ya Serikali (*Public Expenditure Review*);

v) Kuanzishwa kwa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (*IFMS*);

vi) Kuanzishwa kwa kamati ya ukomo;

vii) Kupitishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2005;

viii) Kupitishwa kwa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa mali za Serikali ya mwaka 2005.

Mhe. Spika, taratibu hizi zimeleta mafanikio ya aina mbali mbali ikiwa ni pamoja na kukuza ushirikishwaji wa wadau, kuoanisha mipango na uwezo wa kuilipia, kuoanisha mipango, rasilimali na utekelezaji wa malengo ya MKUZA na Milenia, pamoja na kuwepo kwa tathmini za mara kwa mara juu ya utekelezaji. Mafanikio haya yamepelekea rasilimali kuelekezwa zaidi katika maeneo yenye tija, kijamii na kiuchumi. Aidha, hatua hizi zimeweza kuimarisha ukusanyaji wa mapato na matokeo yake ni kuongezeka kwa

ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa asilimia 356.7 kutoka Tsh 39,157 milioni mwaka 2000/2001 hadi Tsh 139,693 milioni mwaka 2008/09.

Mhe. Spika, Dira ya 2020 imesisitiza juu ya Mageuzi ya Uchumi kuelekea uchumi unaongozwa na uzalishaji viwandani, utalii endelevu na kilimo cha kisasa. Katika kipindi hichi Serikali imeimarisha sekta ya utalii ambayo ni moja katika sekta kiongozi katika uchumi wa Zanzibar kwa kutunga sheria mpya ya Utalii Nam. 6 ya 2009 ili kurahisisha utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Utalii na Sera ya Utalii. Pia machapisho yenye kuitangaza Zanzibar katika lugha za Kifaransa, Kichina, Kirusi, Kijerumani, Kitaliana, Kispaniola na Kiingereza yametolewa ili kuwarahisishia watalii kupata taarifa za Zanzibar. Pia vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi vilialikwa na kuandika makala zenye kuitangaza Zanzibar. Utekelezaji wa mikakati hiyo ya utangazaji imeiwezesha Zanzibar katika kipindi cha mwaka 2000-2009 kutembelewa na watalii 1,100,463. Hoteli 12 za Nyota Tatu, 11 za Nyota Nne na 11 za Nyota Tano zimejengwa na zinaendelea kutoa huduma.

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya biashara na viwanda – Sera ya Uendelezaji wa Biashara/Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati SME's imekamilika na kutafsiriwa katika lugha nyepesi. Viwanda saba vimeanzishwa na kiwanda kimoja cha sukari kinaendelea kufufuliwa. Serikali imeunda Baraza la Biashara la Zanzibar lenye wajumbe kutoka sekta ya umma na sekta binafsi na tayari limeshafanya vikao vinne kwa mafanikio makubwa pamoja na kuimarisha majadiliano yaliyosaidia kupunguza migongano. Pia Serikali imekamilisha uundaji wa Mkakati wa Usafirishaji Bidhaa *(Zanzibar Export Strategy).*

Mhe. Spika, miundombinu ya barabara zenye kilomita 270.5 Unguja na Pemba, Gati ya Malindi Unguja, upanuzi wa gati na ujenzi wa ukuta wa kuzuia mmong'onyoko kwa gati ya Wesha zimekamilika. Matengenezo ya barabara ya kurukia na kutulia ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar yapo katika hatua ya mwisho kukamilika. Aidha, mradi wa umeme Pemba kutoka Tanga nao umekamilika. Wakati huo huo ununuzi wa majenereta ya umeme wa akiba kwa Unguja nao pia umefanyika. Serikali imefanikiwa kusambaza huduma ya umeme katika vijiji 141 kote Unguja na Pemba. Kati yake, vijiji 73 vilikuwa vya Unguja na vijiji 68 vya Pemba.

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya maji, katika mwaka 2000, kiwango cha jumla cha upatikanaji wa maji kwa vijijini kilikuwa asilimia 41. Juhudi za kujenga miradi 32 kwa Unguja na miradi 33 kwa Pemba ziliweza kuinua kiwango cha upatikanaji maji vijijini hadi kufikia asilimia 60. Uimarishaji wa huduma ya maji katika maeneo ya mijini (Unguja mjini, Chake- Chake, Wete

na Mkoani) yalisaidia kuinua kiwango cha upatikanaji maji kutoka asilimia 70 katika mwaka 2000 hadi asilimia 80 mwaka 2010.

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya kilimo, skuli za wakulima zimeanzishwa katika wilaya za Unguja na Pemba kupitia Mipango ya Kuendeleza Huduma za Kilimo na Mifugo *(ASSP na ASDP-L)* na kupatiwa mafunzo ya kilimo na ufugaji. Miundombinu ya umwagiliaji imeimarishwa katika mabonde ya Kibokwa na Bumbwisudi. Aidha, jumla ya matrekta 45 sawa na asilimia 83 ya mahitaji yamenunuliwa. Vile vile utafiti wa mbegu za mazao umefanywa ambapo jumla aina 100 za mbegu za mpunga (*NERICA*) zimefanyiwa majaribio. Serikali pia imenunua mtambo mpya wa *Liquid Nitrogen* ili kuendeleza kazi za upandishaji ng'ombe kwa njia ya sindano na sekta ya uvuvi imeendelea kutoa vifaa mbali mbali vya uvuvi.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Elimu, elimu ya awali (maandalizi) imeendelea kupanuka kwa kuongezeka kwa idadi ya skuli na wanafunzi. Hivi sasa elimu hii inatolewa katika skuli 232 zikiwemo 32 za Serikali na 200 za watu binafsi.

Mhe. Spika, Serikali imeendelea kutoa elimu ya msingi katika skuli 167 za msingi ambazo ni sawa na asilimia 134 baina ya mwaka 2000 na 2009. Vile vile skuli 123 za msingi na kati, zikiwemo 36 za watu binafsi sawa na ongezeko la asilimia 41.9 kutoka mwaka 2000 hadi mwaka 2009. Idadi ya wanafunzi imefikia 220,819 sawa na asilimia 106.8 ya watoto wenye umri wa miaka 7 hadi 13 ambao wanapaswa kuwepo katika ngazi hii ya elimu kutoka asilimia 94.6 mwaka 2001. Mafunzo ya ualimu yamekuwa yakitolewa kwa walimu wa masomo yote ya msingi katika vituo vya walimu kwa lengo la kuwaendeleza kitaalamu.

Mhe. Spika, Serikali imerekebisha mfumo wa utoaji wa elimu ya juu kwa kuimarisha matumizi ya fursa zilizopo na zitakazoongezwa kwa kuanzisha Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*) mwaka 2001 kikiwa na wanafunzi 53 wanaochukua Shahada ya Kwanza ya Sanaa na Elimu. Hivi sasa chuo kina wanafunzi 399 wanaochukua shahada ya kwanza ya Ualimu Sanaa, Ualimu Sayansi na Kompyuta. Aidha, vyuo vikuu vyengine viwili vimeanzishwa na sekta binafsi. Aidha, vituo viwili vya mafunzo ya amali na kimoja cha elimu mbadala vimejengwa Unguja na Pemba.

Aidha, Serikali imeanzisha Mfuko wa Elimu ya Juu kwa lengo la kutoa mikopo kwa ajili ya masomo kwa vijana wanaokwenda masomoni ndani na nje ya nchi. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2001, mfuko umetoa mikopo kwa vijana 2,025 katika fani mbalimbali za masomo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Afya, Serikali inaendelea kuimarisha huduma kwa wananchi wote kwa kuweka sera na mikakati mbali mbali. Malaria ni moja kati ya maradhi yanayosumbua sana hapa nchini katika nchi zinazoendelea hasa zilizo katika Ukanda wa Joto hususan zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Serikali imefanikiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa ugonjwa wa malaria kwa kufikia chini ya asilimia moja kupitia kampeni yake ya KATAA MALARIA. Hivi sasa Serikali inaelekea katika kampeni ya MALIZA KABISA MALARIA ZANZIBAR.

Aidha, SMZ imeendelea na jitihada za kuimarisha afya za mama wajawazito pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na kupunguza vifo vya watoto waliochini ya umri wa miaka mitano. Uzinduzi wa Mkakati wa Kupunguza Vifo vya Mama na Mtoto umefanyika na huduma mbali mbali juu ya uzazi wa mpangilio zimetolewa.

Mhe. Spika, kuhusu mapambano dhidi ya ukimwi Serikali inaendelea kutoa elimu kwa makundi mbali mbali, wafanyakazi katika sekta zote, familia na wana jamii, ili kupunguza na hatimae kuondosha kabisa tatizo la ukimwi. Aidha, huduma za tiba za *ARV* zilianzishwa kwa lengo la kuwafanya waathirika waishi kwa matumaini zaidi kwa utoaji wa dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI. Serikali pia imezindua kampeni dhidi ya unyanyapaa kwa waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI.

Mhe. Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mnazimmoja inaendelea kuimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi vya kisasa kama vile *machine* za *X-ray*, *CT Scan*, *Fluoroscopy*, *Ultrasound na Echo Cardiography* pamoja na vifaa vya kuhudumia macho na viungo.

Hospital ya Wete nayo pia imepatiwa umeme wa mionzi ya jua na sehemu ya kuhifadhia damu salama. Hospitali ya Chakechake imepatiwa mashine ya kuchunguza virusi vya ukimwi pamoja na mashine ya kuangalia mwenendo wa damu kwenye moyo (*ECG*) na vifaa mbali mbali vya upasuaji. Madarasa mawili ya madaktari wanafunzi yanayoendeshwa na walimu kutoka Cuba yamefunguliwa, moja Unguja na jengine Pemba. Aidha, Chuo cha Afya Mbweni kimetanuliwa na kuongezwa madarasa ili kuweza kukidhi mahitaji ya makubwa ya wataalamu kwenye Sekta ya Afya.

MAPITIO YA HALI YA UCHUMI DUNIANI NA KIKANDA

Mhe. Spika, kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Fedha Duniani, uchumi wa dunia wa mwaka 2009 ulishuka kwa wastani wa asilimia 0.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.0 kwa mwaka 2008. Hali hii imechangiwa zaidi na msukosuko wa fedha ambao umeathiri ukuaji wa uchumi wa mataifa mbali

mbali duniani. Ukuaji wa uchumi kwa mataifa makubwa umeshuka kwa wastani wa asilimia 3.2 kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 0.5 kwa mwaka 2008.

Mhe. Spika, uchumi wa nchi zinazoendelea umekuwa kwa wastani wa asilimia 2.4 kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.1 mwaka 2008. Uchumi wa nchi zinazoendelea katika bara la Asia umekuwa kwa asilimia 6.6 kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.9 kwa mwaka 2008.

Mhe. Spika, kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, uchumi wake umekuwa kwa wastani wa asilimia 2.1 kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.5 ya mwaka 2008. Uchumi wa nchi za Afrika ya Mashariki kwa mwaka 2009 ulikua kwa wastani wa asilimia 4.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.8 mwaka 2008.

Mhe. Spika, moja kati ya eneo muhimu katika usimamizi wa uchumi ni kuhakikisha kuwepo kwa utulivu wa bei na hivyo haja ya kudhibiti mfumko wake. Kwa mwaka 2009, mfumko wa bei kwa nchi za Afrika umefikia asilimia 10.7. Katika mwaka huo, mfumko wa bei kwa baadhi ya nchi barani Afrika kama vile Rwanda ulifikia asilimia 11.5, Uganda asilimia 14.2, Kenya asilimia 12.0, Afrika ya Kusini asilimia 7.1 na Tanzania Bara asilimia 12.1. Mfumko huo kwa kiwango kikubwa ulisababishwa na ongezeko la bei za vyakula.

MAPITIO YA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR

Pato la Taifa na Ukuaji wake

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009 Pato la Taifa lilifikia thamani ya TZS 878,403 milioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 748,057 milioni kwa mwaka 2008. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 17.4 kwa bei za miaka husika (*current prices*). Kiwango hiki cha ukuaji wa Pato la Taifa kimesababisha mafanikio katika kasi ya ukuaji halisi wa hali ya uchumi kufikia asilimia 6.7 kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.3 iliyofikiwa mwaka 2008. Awali, kwa sababu za msukosuko wa fedha duniani, ukuaji halisi wa uchumi Zanzibar ulitarajiwa kufikia asilimia 4.9 kwa mwaka 2009. Baadhi ya vichocheo vikuu vya ukuaji huu ni pamoja na mambo yafuatayo:-

a) Mageuzi katika Sekta ya Kilimo yaliyokwenda sambamba na hali nzuri ya hewa iliyopelekea kuimarika kwa shughuli za kilimo;

b) Ongezeko katika jumla ya thamani ya uwekezaji rasilimali kwa asilimia 21 kutoka TZS 145,151 milioni kwa mwaka 2008 hadi kufikia TZS 175,877 milioni kwa mwaka 2009; na

c) Kuongezeka idadi ya watalii walioingia nchini kutoka 128,445 kwa mwaka 2008 hadi kufikia 134,954 kwa mwaka 2009 sawa na ongezeko la asilimia 5.1.

Mhe. Spika, kuongezeka kwa thamani ya Pato la Taifa kumepelekea kiwango cha wastani wa Pato la Mtu kwa bei za miaka husika (*current prices*) kupanda hadi kufikia Dola za Kimarekani 557 (sawa na TZS 728,361) kutoka thamani ya Dola za Kimarekani 534 (sawa na TZS 638,819) kwa mwaka 2008, ikiwa ni sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 4.3.

UKUAJI WA SEKTA

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2009, Sekta ya Huduma imekuwa kwa asilimia 8.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.1 kwa mwaka 2008. Hali hii imetokana na ukuaji katika shughuli za Usafiri na Mawasiliano ambazo zimeongezeka kwa asilimia 22.1 kwa mwaka 2009. Aidha, shughuli nyengine zilizokuwa na ongezeko kubwa ni: afya asilimia 7.9, elimu asilimia 5.6, hoteli na mikahawa asilimia 5.0. Shughuli za kibiashara nazo zimekuwa kwa asilimia 4.0 ikilinganishwa na kushuka kwa asilimia 4.3 mwaka 2008.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Kilimo, kasi ya ukuaji imeshuka kidogo kutoka asilimia 5.7 kwa mwaka 2008 na kufikia ukuaji wa asilimia 4.4 kwa mwaka 2009. Hali hii imesababishwa na kupungua kwa uzalishaji wa mazao hasa ya biashara kama vile karafuu ambapo tani 4,007 zilizalishwa mwaka 2008 wakati mwaka 2009 tani 3,536 zilizalishwa. Aidha, katika kipindi hicho uzalishaji wa mwani nao ulipungua kidogo kutoka tani 11,177 kwa mwaka 2008 hadi kufikia tani 10,248 kwa mwaka 2009. Katika kipindi hiki kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula kwa asilimia 14.3, baadhi ya mazao ambayo uzalishaji wake umeongezeka ni muhogo, mahindi, mpunga na viazi vikuu.

Mhe. Spika, uzalishaji viwandani umepanda kwa kasi zaidi kutoka ukuaji wa asilimia 1.1 kwa mwaka 2008 na kufikia ukuaji wa asilimia 2.4 kwa mwaka 2009. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa uzalishaji bado inahitaji kupanda kwa haraka zaidi ili viwanda viweze kuchangia kiwango kikubwa katika pato la taifa kama inavyohitajika katika Dira ya Maendeleo ya 2020.

MCHANGO WA SEKTA KATIKA PATO LA TAIFA

Mhe. Spika, mchango wa Sekta ya Huduma kwa Pato la Taifa ulifikia asilimia 44.0 kwa mwaka 2009 ukiwa umepanda kutoka mchango wa asilimia 42.7 kwa mwaka 2008. Shughuli za kiuchumi ambazo zimechangia katika sekta ya utoaji huduma ni Mawasiliano na Uchukuzi ambazo zilichangia kwa asilimia 11.0 kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 8.0 kwa mwaka 2008. Aidha, mchango wa shughuli za kibiashara umepungua hadi kufikia asilimia 8.4 kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 8.7 kwa mwaka 2008.

Mhe. Spika, mchango wa Sekta ya Kilimo kwenye Pato la Taifa umeongezeka ambapo mwaka 2009 imechangia asilimia 30.8 ikilinganishwa na asilimia 30.7 ya mwaka 2008. Shughuli za uzalishaji wa mazao zilichangia asilimia 20.8 ikilinganishwa na asilimia 21.3 ya mwaka 2008. Aidha, shughuli za uvuvi nazo zilichangia asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.4 kwa mwaka 2008.
Mhe. Spika, mchango wa sekta ya viwanda ambayo inahusisha uzalishaji viwandani, ujenzi, miundombinu ya umeme na maji pamoja na uchimbaji wa mawe, inaonesha kushuka kwa mchango wake kutoka asilimia 14.3 mwaka 2008 na kufikia asilimia 13.1 mwaka 2009. Kushuka kwa mchango wa sekta hii kunatokana na ukuaji mkubwa zaidi katika mchango wa sekta ya huduma kuliko ilivyokuwa kwa sekta ya viwanda.

UKUZAJI RASILIMALI

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009 ukuzaji rasilimali umeongezeka kwa thamani ya TZS 30,726 milioni ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 21.2 kutoka TZS 145,151 milioni kwa mwaka 2008 hadi TZS 175,877 milioni kwa mwaka 2009. Ongezeko hili la thamani limetokana na uwekezaji mkubwa kwa upande wa serikali katika ujenzi wa barabara na miundombinu mingine ya kiuchumi na kijamii pamoja na Sekta Binafsi katika maeneo ya ujenzi wa nyumba za kuishi na za biashara.

Mhe. Spika, uwekezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja na ardhi, umekua kwa asilimia 14.6 kutoka TZS 51,398 milioni mwaka 2008 hadi TZS 58,935 milioni mwaka 2009. Uwekezaji katika vifaa vya usafirishaji na mitambo umekua kwa asilimia 38.8 katika kipindi hicho kutoka TZS 44,199 milioni hadi TZS 61,368 milioni.

UWEKEZAJI BINAFSI

Mhe. Spika, kiwango cha uwekezaji binafsi kilishuka kutoka Dola za Kimarekani 1,296.8 milioni kwa mwaka 2008 na kufikia Dola za Kimarekani 270.4 milioni kwa mwaka 2009. Upungufu huu umetokana na uwekezaji mdogo, ambapo jumla ya miradi iliyowekezwa ilipungua kutoka miradi 65

kwa mwaka 2008 na kufikia miradi 34 kwa mwaka 2009. Kushuka huko kwa uwekezaji kumetokana na kupungua kwa uwekezaji katika miradi ya utalii ambapo miradi ya ujenzi wa hoteli na mikahawa ilifikia miradi 15 mwaka 2009 ikilinganishwa na miradi 46 mwaka 2008.

MFUMKO WA BEI

Mhe. Spika, kiwango cha mfumko wa bei kwa mwaka 2009 kilishuka na kufikia asilimia 8.9 mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 20.6 kwa mwaka 2008. Mafanikio haya yamepindukia matarajio ya mfumko wa asilimia 13 kwa mwaka 2009. Sababu kuu zilizosababisha kupungua kwa kasi hii ni tatu:-

- Hali nzuri ya hewa ambayo ilisababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula nchini;
- Kupungua kwa bei za baadhi ya vyakula vinavyoagizwa nje ya nchi hasa bidhaa ya mchele; na
- Kupungua kwa bei za mafuta katika soko la dunia mwishoni mwa mwaka 2008 na mwanzoni mwa mwaka 2009.

MIZANIA YA BIASHARA

Mhe. Spika, bidhaa zenye thamani ya TZS 29,744.5 milioni zilisafirishwa na kuuzwa nje kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya TZS 30,189.2 milioni kwa mwaka 2008. Usafirishaji huu umepungua kwa asilimia 1.5. Hali hii ilisababishwa na upungufu wa usafirishaji wa mazao ya asili ya karafuu na mwani, ambapo kwa mwaka 2009 jumla ya tani 3,103 za karafuu zenye thamani ya TZS 14,077 milioni ziliuzwa nje ikilinganishwa na tani 3,449 zenye thamani ya TZS 15,878 milioni zilizouzwa mwaka 2008. Kwa upande wa zao la mwani, jumla ya tani 9,416 zenye thamani ya TZS 3,013 milioni ziliuzwa nje kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na tani 11,905 zenye thamani ya TZS 3,492 milioni kwa mwaka 2008.

Mhe. Spika, kwa upande wa uingizaji kutoka nje ya nchi, bidhaa zenye thamani ya TZS 120,882.0 milioni ziliagizwa mwaka 2009 ikilinganishwa na TZS 93,439.6 milioni kwa mwaka 2008. Kuongezeka kwa uagiziaji kumesababisha kuongezeka kwa nakisi katika urari wa biashara ambapo nakisi hio imeongezeka kutoka jumla ya TZS 63,250.4 milioni kwa mwaka 2008 na kufikia TZS 91,137.5 milioni kwa mwaka 2009.

Mhe. Spika, biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara iliendelea kufanyika ambapo bidhaa zenye thamani ya TZS 19,651.0 milioni ziliingia Zanzibar kutoka Tanzania Bara kwa mwaka 2009 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya TZS 25,936.6 milioni kwa mwaka 2008. Kumekuwa na ongezeko la bidhaa zinazohaulishwa kutoka Zanzibar kuelekea Tanzania Bara ambapo

bidhaa zenye thamani ya TZS 4,256.6 milioni zilihaulishwa mwaka 2009 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya TZS 2,938.7 milioni mwaka 2008. Mwenendo huu wa biashara kati ya sehemu hizi mbili za Jamhuri ya Muungano kwa mwaka 2009 umeweza kupunguza kiwango cha nakisi kutoka jumla ya TZS 24,456.8 milioni mwaka 2008 na kufikia TZS 18,309.9 milioni kwa mwaka 2009 kwa bidhaa zinazozalishwa nchini.

HUDUMA ZA FEDHA

Mchango wa Sekta ya Fedha katika Uchumi wa Zanzibar

Mhe. Spika, Sekta ya Fedha ni muhimili muhimu katika uchumi ikiwa na jukumu la kukusanya amana na kutoa mikopo katika sekta mbali mbali. Idadi ya benki za biashara imeongezeka kutoka sita mwezi Machi mwaka 2009 hadi kufikia kumi mwishoni mwa mwezi wa Machi 2010. Ukusanyaji na uwekaji wa amana (*deposits*) katika benki za biashara nao umeongezeka kwa asilimia 36.1 hadi kufikia TZS 264,100 milioni mwezi Machi 2010 kutoka TZS 194,000 milioni mwezi Machi 2009. Uwiano wa uwekaji wa amana kwa Pato la Taifa (*Deposit to GDP ratio*) ulifikia asilimia 30.1 hadi Machi 2010 toka asilimia 22.1 Machi 2009.

Mhe. Spika, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka hadi kufikia TZS 80,900 milioni mwezi Machi 2010, kutoka shilingi 62,400 milioni mwezi Machi 2009 ikiwa ni wastani wa ongezeko la asilimia 29.6. Ukuaji wa ukopeshaji kwa sekta binafsi na pato la taifa ulifikia wastani wa asilimia 9.2 mwezi Machi 2010 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.1 mwezi Machi 2009. Hii inaashiria kukua kwa shughuli za kibiashara na uchumi Zanzibar. Kati ya mikopo iliyotolewa, kiasi cha asilimia 55.9 ilikwenda kwa watu binafsi *(personal loans*). Sekta ya Utalii ilipokea asilimia 14.4, biashara asilimia 5.1 na ujenzi asilimia 3.0.

DENI LA TAIFA

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2010, Deni la Taifa lilifikia jumla ya TZS 145,023 milioni sawa na asilimia 16.5 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na TZS 136,575 milioni kwa mwezi Machi 2009. Kati ya deni hilo TZS 83,787 milioni sawa na asilimia 58 ni deni la nje na TZS 61,235 milioni sawa na asilimia 42 ni deni na ndani.

Mhe. Spika, deni la nje la TZS 83,787 milioni linajumuisha deni lililodhaminiwa na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo ni TZS 62,811 milioni. Deni hilo limeongezeka kwa asilimia 5 ikilinganishwa na deni lilodhaminiwa na SMT mwezi Machi, 2009. Sababu kuu ya kuongezeka

kwa deni hilo ni mabadiliko ya thamani ya sarafu ya Tanzania na za kigeni. Aidha, TZS 20,976 milioni zimedhaminiwa na SMZ ambazo zimeongezeka kwa asilimia 4 ikilinganishwa na deni la Machi, 2009. Sababu kuu ya ongezeko la deni hilo ni mabadiliko ya thamani ya sarafu ya Tanzania na za Kigeni.

Mhe. Spika, deni la ndani la TZS 61,235 milioni linalojumuisha mikopo, hati fungate, wazabuni, madeni ya mashirika pamoja na kiinua mgongo limeongezeka kwa asilimia 8 ikilinganishwa na deni la Machi, 2009. Sababu kuu ya kuongezeka kwa deni hilo ni mkopo wa hati fungate (*Treasury Bond*) uliochukuliwa na serikali.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 deni la kiinua mgongo na mafao ya wastaafu wa serikali lililokusanywa lilifikia TZS 6,396 milioni. Malipo ya TZS 5,797 milioni yalifanyika katika kipindi hicho na kufanya deni halisi la mafao ya kiinua mgongo hadi Machi, 2010 kufikia TZS 599 milioni.

AJIRA ILIYO RASMI NCHINI

Mhe. Spika, idadi ya waajiriwa imekuwa ikiongezeka ndani ya Sekta ya Umma na ile ya binafsi ambapo idadi ya waajiriwa imefikia watu 47,551 mwaka 2009 kutoka waajiriwa 41,608 mwaka 2008 sawa na ongezeko la asilimia 13.7. Kati ya waajiriwa hawa jumla ya wafanyakazi 31,378 sawa na asilimia 75.5 wamo katika Sekta ya Umma ambapo asilimia 40.0 kati yao wamo katika Sekta ya Elimu. Aidha, wafanyakazi wa Sekta Binafsi wamefikia 10,230 sawa na asilimia 24.5 ya waajiriwa wote. Kati ya hao asilimia 12.8 wanafanya kazi katika shughuli mbali mbali katika Sekta ya Utalii. Idadi ya wafanyakazi wanaume ni kubwa ikilinganishwa na ile ya wanawake kwa asilimia 19.4.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2009/2010

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2009/2010 ulilenga kutekeleza jumla ya programu 22 na miradi 65. Jumla ya TZS 239,913 milioni zilipangwa kugharamia programu na miradi hiyo ikijumuisha mchango wa serikali TZS 40,725 milioni na misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo TZS 199,188 milioni.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa (Julai, 2009-Machi, 2010) jumla ya TZS 95,277 milioni zilitolewa sawa na asilimia 50.3 ya makadirio ya mwaka.

Kati ya fedha hizo, TZS 28,291 milioni sawa na asilimia 69.5 zilitolewa na serikali na TZS 66,986 milioni sawa na asilimia 46.4 ni mchango wa Washirika wa Maendeleo. Idadi hiyo ya fedha haijumuishi TZS 25,931 milioni zilizotolewa na Washirika wa Maendeleo kwa miradi ambayo haikuwemo ndani ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2009/2010 na kufanya fedha zilizotolewa na Washirika wa Maendeleo kufikia TZS 92,917 milioni. Ufuatao ni muhtasari wa utekelezaji kwa kila Klasta ya MKUZA.

KLASTA YA UKUZAJI UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASIKINI WA KIPATO

Mhe. Spika, Klasta ya Ukuzaji Uchumi na Kupunguza Umasikini wa Kipato kwa mwaka 2009/2010, ilikuwa na programu 14 na miradi 21. Klasta hii ilipangiwa kutumia TZS 145,724 milioni sawa na asilimia 61 ya bajeti ya maendeleo, kutekeleza programu 14 na miradi 21 ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, TZS 23,729 milioni zilipangwa kutolewa na serikali ikiwa ni asilimia 58.3 ya mchango wake katika bajeti yote ya maendeleo. TZS 121,995 milioni zilizobakia zilitarajiwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 61.3 ya mchango wao.

Mhe. Spika, kuanzia Julai, 2009 mpaka Machi, 2010, TZS 65,575 milioni sawa na asilimia 45 ya bajeti ya maendeleo kwa klasta ya kwanza zimetolewa. Kati ya fedha hizo serikali imetowa TZS 13,020 milioni sawa na asilimia 68 ya makadirio ya mchango wake na Washirika wa Maendeleo wamechangia TZS 52,554 milioni sawa na asilimia 43 ya makadirio ya mchango kutoka kwao.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi katika klasta hii ulikwenda vizuri ambapo pamefanyika mapitio ya utaratibu wa utunzaji wa mali za serikali chini ya programu ya mageuzi katika Usimamizi wa Fedha za Umma. Vile vile, Mpango wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA) unaendelea kutekelezwa kwa kufanya mageuzi katika Eneo la Kodi.

Uratibu wa Misaada

Mhe. Spika, uratibu wa misaada kwa miradi ya serikali na taasisi zisizo za kiserikali umeendelea kufanyika, ambapo jumla ya miradi 13 imewasilishwa kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya ufadhili kwa kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010. Ili kuwasaidia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupata uelewa mzuri wa taratibu za misaada, nao pia wamepatiwa mafunzo ya Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA).

Ujenzi wa Barabara

Mhe. Spika, serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi inayolenga kuimarisha barabara hususan za vijijini ambako ndiko kwenye uzalishaji wa kilimo. Jumla ya barabara 13 zenye urefu wa kilomita 121.6 zinaendelea kujengwa Unguja na Pemba. Barabara hizo ni Wete-Chake, Wete-Konde, Wete-Gando, Mtambile-Kengeja, Mtambile-Kangani, Mizingani-Wambaa, Kenya- Chambani, Tundauwa-Pujini, Amani-Dunga, Mfenesini-Bumbwini, Chanjamjawiri-Tundauwa na Chanjaani-Pujini. Aidha, barabara ya Mazizini-Fumba na Kinyasini-Tunguu nazo zimekamilika. Hatua za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Ole-Kengeja yenye urefu wa kilomita 35 nazo zinaendelea. Barabara zinazoendelea kufanyiwa matengenezo ni Mgagadu-Kiwani, Kangani-Mkanyageni na Pale- Kiongole.

Nishati

Mhe. Spika, umuhimu wa nishati ya umeme kwa maendeleo ya uchumi na huduma za jamii hauhitaji kuelezwa zaidi. Awali niliahidi kutoa maelezo zaidi juu ya hatua zilizochukuliwa na serikali kukabiliana na tatizo la kukosekana kwa umeme lilipojitokeza na kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa kisiwa cha Unguja. Naomba sasa nitoe maelezo hayo.
Mhe. Spika, katika juhudi za kuepusha tatizo hilo lisitokee tena, serikali imechukua hatua kadhaa kuunganisha na zile zilizopo za muda mrefu. Hatua zinazoendelea kutekelezwa ni tatu kama ifuatavyo:-

(a) Mpango wa muda mfupi – ulilenga katika kurejesha kwa haraka huduma hiyo kwa kufanya matengenezo katika vituo vidogo vya umeme huko Ras Kiromoni, Tanzania Bara na kituo cha kupokelea umeme cha Ras Fumba hapa Zanzibar. Matengenezo haya yalihusisha kuweka mfumo mpya wa kutumia na kupokelea umeme ili kuondokana na mfumo uliokuwepo zamani ambao ndio uliosababisha uharibifu mara mbili ndani ya miaka miwili ; na

(b) Mpango wa muda wa kati – mpango huu umelenga katika upatikanaji wa umeme wa akiba litapotokezea tatizo katika '*Grid'* ya taifa. Mpango huu umehusisha ununuzi wa majenereta mapya thelathini na mbili (32) yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya megawati 25 za umeme. Hatua ya ufungaji wa majenereta haya inaendelea vizuri na inatarajiwa kukamilika kabla ya tarehe 30 Juni, 2010.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya serikali na wananchi wote wa Zanzibar, kuzishukuru sana nchi za Norway, Sweden na Uingereza

kwa msaada wao wa dharura wa fedha na utaalam uliofanikisha ununuzi wa majenereta haya. Mradi huu mpaka utakapomalizika unatarajiwa kugharimu jumla ya Dola za Kimarekani 13 milioni, sawa na TZS 17,810 milioni ambapo Norway imechangia Dola za Kimarekani milioni 4, Sweden Dola milioni 4.5 na Uingereza Dola milioni 3. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechangia Dola milioni 1.5 kuweza kukamilisha gharama zinazohitajika za Dola 13 milioni kwa ununuzi, usafirishaji na ufungaji wa majenereta hayo.

c) Mpango wa muda mrefu – Mpango huu ulilenga kuweka njia mpya ya umeme chini ya bahari kutoka Dar Es Salaam hadi Unguja. Njia hii itakayofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Changamoto za Milenia *(MCC),* itakuwa na uwezo mkubwa zaidi kuliko ile ya sasa. Njia iliyopo hivi sasa ina nguvu za 45 MW wakati njia mpya itayojengwa itakuwa na uwezo wa 100 MW. Matayarisho juu ya uwekaji wa njia hiyo inayotarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2012 yanaendelea vizuri. Mkataba wa ujenzi tayari umeshatiwa saini tokea tarehe 30 Aprili, 2010. Matayarisho ya kulipwa fidia kwa wananchi watakaoathirika baina ya Fumba na kituo kikuu cha umeme Mtoni nayo yamekamilika.

Mhe. Spika, katika uendelezaji wa Sekta hii upatikanaji wa nishati ya umeme kwa uhakika ni moja ya ahadi muhimu katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Mkakati huu unahusisha pia kukipatia kisiwa cha Pemba umeme wa uhakika kwa kukiunganisha na mfumo wa Taifa kupitia mkongo wa chini ya bahari.

Mhe. Spika, kwa fakhari kubwa nina furaha kuweka katika kumbukumbu kuwa ahadi hiyo ya Chama Tawala cha CCM iliyomo ndani ya Ilani ya Uchaguzi sasa imetimizwa. Kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, Wananchi wa Pemba sasa wananufaika na huduma hiyo ya umeme wa kuaminika. Hatimae umeme kutoka Tanga kupitia chini ya bahari unawaka Pemba. Naomba nichukue fursa hii kuwashukuru tena na kwa dhati kabisa Wananchi wote hasa wakaazi wa Kisiwa cha Pemba kwa ustahamilivu wao wa muda mrefu wa kutokuwa na uhakika wa huduma hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba pia nitoe shukrani maalum kwa Wananchi na Serikali ya Norway na Ubalozi wake uliopo hapa nchini kwa msaada wao mkubwa wanaoendelea kuipatia nchi yetu katika sekta hii ya nishati, ikiwemo mchango wao mkubwa wa NOK 300 milioni sawa na Dola za Kimarekani 50 milioni ikiwa ni asilimia 77 ya gharama zote za mradi huu. Tunamshukuru pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mchango wao wa

Dola za Kimarekani milioni tano sawa na asilimia 8 ya gharama za mradi. Pia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wake imechangia jumla ya Dola za Kimarekani 10 milioni sawa na asilimia 15 ya gharama zote za mradi.

Kilimo

Mhe. Spika, Sekta ya Kilimo ina nafasi maalum katika maendeleo na ustawi wa uchumi na wananchi. Kutokana na kilimo ndio tunazalisha mazao ya chakula na biashara, tunapata malighafi kwa ajili ya uzalishaji viwandani, pia nchi inapata fedha za kigeni kutokana na mauzo ya mazao nje, na kupata rasilimali watu kwa ajili ya uzalishaji katika sekta nyengine. Katika kipindi hiki**,** mafunzo na ushauri wa kuwashajihisha wakulima katika uzalishaji wa mazao ya chakula kupitia kilimo cha umwagiliaji yametolewa. Aidha, ushajihishaji na mafunzo ya kumwagilia kwa njia ya matone *(drip irrigation)* yametolewa kwa wakulima wenye uwezo wa kununua vifaa vya matumizi katika maeneo ya Zingwe Zingwe, Makunduchi na Bumbwisudi. Sekta hii imefanikiwa kuzalisha jumla ya tani 88 za mbegu bora za mpunga zenye thamani ya TZS 70 milioni zilizonunuliwa kutoka kwa wakulima kupitia Skuli za Wakulima, hivyo kufikia lengo la kuzalisha mbegu bora za mpunga kwa asilimia 88. Jitihada za kuyapatia ufumbuzi matatizo ya nzi wa matunda *(spiral white flies)* na wadudu wengine waharibifu zinaendelea kuchukuliwa katika mashamba ya wakulima kwa kutumia dawa za asili na dawa nyenginezo.

KLASTA YA HUDUMA NA USTAWI WA JAMII

Mhe. Spika, masuala yote ya Huduma na Ustawi wa Jamii yamewekwa pamoja katika Klasta ya Huduma na Ustawi wa Jamii. Klasta hii inahusisha masuala ya afya, elimu, maji safi na salama, maji taka, makaazi bora na uhifadhi jamii. Kwa mwaka 2009/2010 Klasta hii ilipangiwa kutumia TZS 80,419 milioni sawa na asilimia 33.5 ya bajeti yote ya maendeleo kwa kutekeleza programu tatu na miradi 28. Kati ya fedha hizo, TZS 9,664 milioni sawa na asilimia 23.7 ni mchango wa serikali na TZS 70,755 milioni sawa na asilimia 35.5 ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2009 - Machi 2010, jumla ya TZS 19,858 milioni sawa na asilimia 24 ya bajeti ya maendeleo zimetolewa. Kati ya fedha hizo Serikali imetoa TZS 9,620 milioni sawa na asilimia 68 ya makadirio ya mchango wake na Washirika wa Maendeleo wamechangia TZS 10,238 milioni sawa na asilimia 15 ya makisio ya mchango wao kwa Klasta hii.

Elimu

Mhe. Spika, Serikali kupitia Sekta ya Elimu imeendelea na juhudi mbali mbali za kuwapatia wananchi elimu bora na yenye manufaa. Hadi kufikia mwezi Machi, 2010 jumla ya miradi 10 yenye thamani ya TZS 4,507 milioni imetekelezwa.

Mhe. Spika, kazi za ujenzi wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) zinaendelea vizuri, hatua zilizofikiwa ni ukamilishaji wa majengo ya Utawala, Maktaba, Sanaa na Sayansi ambapo asilimia 90 ya kazi imekamilika.

Mhe. Spika, chini ya mradi wa elimu ya msingi, jumla ya nakla 2,000 za mihutasari mipya ya elimu ya msingi zimechapishwa kwa masomo 15 kuanzia darasa la I–VI. Mafunzo ya Awali kwa walimu 450 wa darasa la kwanza yalifanyika kwa Unguja na Pemba na walimu 36 wamepatiwa mafunzo kazini katika vituo tisa vya ualimu.

Mhe. Spika, Serikali imeendelea kuimarisha Elimu Mbadala na Amali kwa nia ya kuongeza ujuzi na fursa za kuajiriwa na kujiajiri. Vijana 390 wamechaguliwa kujiunga na mafunzo ya amali, wakiwemo 252 kwa kituo cha Mkokotoni na 138 kituo cha Vitongoji. Zana na vifaa kwa ajili ya mafunzo ya kompyuta, utengenezaji magari, upishi na useremala vimefungwa katika vituo hivyo. Ujenzi wa Kituo chengine cha Elimu Mbadala huko Wingwi, Pemba nao tayari umeanza.

Afya

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za afya, Sekta ya Afya imefanya mapitio ya Sera ya Afya ili iende sambamba na sera za taifa na za kimataifa. Miongozo ya Kitaifa ya utoaji huduma za Afya na kusaidia utatuzi wa maradhi imetayarishwa. Jitihada za kuleta mabadiliko ya Sekta ya Afya zinafanywa ambapo jumla ya vituo 34 vimenyanyuliwa hadhi na kuwa Vituo vya Afya Daraja la Pili *(PHCU+).* Hospitali za Mnazimmoja, Wete, Chake Chake, Mkoani zimepata maendeleo makubwa baada ya kupata vitendea kazi kama nilivyotangulia kueleza hapo awali. Aidha, Hospitali ya Mnazimmoja imeanzisha huduma za haraka za matibabu *(fast track).*

Mhe. Spika, Hospitali ya Ugonjwa wa Akili, Kidongochekundu inaendelea kuimarishwa kwa kufanyiwa matengenezo kwa ufadhili wa Bwana Al-Gurg wa Dubai, Falme za Kiarabu. Ujenzi huo unategemewa kumalizika mwaka huu wa 2010. Sehemu zilizojengwa na ambazo zimekamilika ni pamoja na Ofisi ya Utawala, sehemu ya wagonjwa wa nje na jiko.

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za afya ya uzazi, Mpango Mkakati wa Kupunguza Kasi ya Vifo umechapishwa. Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa

kushirikiana na vituo vya kinamama na watoto imechukua hatua mbali mbali za kuanzisha huduma za afya ya mama na mtoto. Kampeni ya chanjo ya Pepo Punda imefanyika katika Wilaya tatu za Pemba (Chake Chake, Micheweni na Mkoani). Aidha, kazi za usambazaji wa vifaa na dawa za chanjo umefanyika kwa vituo vyote vya afya vinavyotoa huduma hizo. Kiwango cha huduma za chanjo kimeongezeka kutoka asilimia 84 mwaka 2007/2008 hadi asilimia 86 mwaka 2008/2009. Chanjo mpya ya kuwakinga watoto na maradhi yanayoweza kusababisha homa ya uti wa mgongo *(Meningitis)* na homa ya mapafu *(Pneumonia)* imeanza kutolewa katika vituo vyote vya Unguja na Pemba.

Udhibiti wa Malaria

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema hapo awali, juhudi za kupambana na kuondosha kabisa maradhi ya malaria zimeonesha mafanikio makubwa. Kwa mashirikiano na wananchi imedhihirika kuwa "Zanzibar bila ya malaria" inawezekana. Kazi za uchunguzi wa vimelea vya Malaria kwa kutumia darubini au uchunguzi wa njia ya haraka *(Rapid Diagnostic Test – RDT)* imefikia asilimia 100 katika vituo vya Serikali na Binafsi. Uhakiki wa vimelea kwa njia ya haraka *(RDT)* umefanyika ambapo jumla ya vituo 75 visivyokuwa na darubini vilifanyiwa uhakiki na kupata takwimu za kila mwezi. Mafunzo kwa watendaji 104 (wanawake 60 na wanaume 44) wa Vituo vya Afya vilivyopo katika Mpango wa Kutambua Malaria Mapema *(Malaria Early Epidemic Detection System - MEEDS)* yamefanyika Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, zoezi la upigaji dawa majumbani kwa awamu ya tano limefanyika huko Pemba na Mikoa ya Kusini na Kaskazini Unguja. Kwa Mkoa wa Mjini Magharibi zoezi litafanyika hivi karibuni na litakwenda sambamba na ugawaji wa vyandarua bila ya malipo katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Maji

Mhe. Spika, huduma nyengine muhimu kwa ustawi wa jamii yenye afya ni upatikanaji wa maji safi na salama. Zanzibar imefanikiwa kuwa na fursa ya maji safi na salama kwa asilimia 80 ya wananchi wake wa mijini na asilimia 60 wa vijijini. Hadi kufikia Machi, 2010 programu moja na miradi mitatu imetekelezwa yenye thamani ya TZS 7,247 milioni.

Makazi Bora

Mhe. Spika, tokea Mapinduzi matukufu ya Januari 1964, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiweka mkazo mkubwa katika upatikanaji wa nyumba bora za kuishi kwa ajili ya wananchi wake. Waheshimiwa Wajumbe na Wananchi wote kwa jumla, tumeshuhudia kukamilika kwa Jumba Namba 10 la Michenzani ambalo lilishindikana kukamilishwa kwa miaka mingi iliyopita. Kukamilika kwa jumba hilo kumetoa fursa kwa Serikali kulipa deni la muda mrefu lililokuwa ikidaiwa na wananchi waliovunjiwa nyumba zao kutoa nafasi kwa ujenzi wa majumba ya awali ya maendeleo ya Michenzani. Serikali inawashukuru wananchi hao wote kwa ustahamilivu wao kwa muda wote huo hadi hivi karibuni walipoweza kulipwa nyumba zao. Ujenzi unaendelea kwa Nyumba za Mpapa.

Mhe. Spika, katika kutekeleza sera ya kuwapatia wananchi makaazi bora, Serikali pia iliendelea na kazi za upimaji wa viwanja Unguja na Pemba sambamba na mchakato wa mapitio ya Sera ya Ardhi na Sera ya Mazingira. Jumla ya viwanja 490 vimepimwa ambapo kwa Pemba viwanja vilivyopimwa ni 138 na Unguja ni viwanja 352. Viwanja hivyo ni kwa ajili ya makaazi, biashara, huduma, taasisi na mashamba.

Hifadhi ya Jamii

Mhe. Spika, hifadhi ya jamii ni moja ya eneo muhimu katika kuihami jamii dhidi ya umasikini. Utafiti kuhusu Mfumo wa Hifadhi ya Jamii umekamilika na ripoti yake imezinduliwa. Utafiti huo umeonesha haja ya kuratibu mifumo tofauti ya utoaji wa huduma ya hifadhi ya jamii isiyohusisha uchangiaji ambayo ipo mingi. Mifumo ya uchangiaji inahudumia asilimia 6.6 ya idadi ya watu wote Zanzibar. Utafiti huo utasaidia pia katika uandaaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii kama hatua inayofuata katika kuweka mfumo bora na kuhakikisha huduma inawafikia watu wote wa Zanzibar.

Uwezeshaji Wananchi

Mhe. Spika, Serikali imeendelea na juhudi zake za kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia mikopo kwa kutumia mifuko mbalimbali. Baina ya Julai 2009 hadi Machi 2010, Mfuko wa Kujitegemea umetoa mikopo 463 yenye thamani ya TZS 326 milioni kwa wajasiriamali 3,855, wanawake 2,580 na wanaume 1,275. Aidha, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (JK na AK) umetoa TZS 1,284 milioni kwa watu binafsi wapatao 555 (wanawake 224 na wanaume 331), *SACCOS* nane na vikundi 45 vya wajasiriamali Pemba na Unguja. Ni wajibu wa wale wote walionufaika na mikopo hiyo kuitumia vyema kwa kujiendeleza na kuirejesha kwa wakati ili lengo la kuwajengea uwezo kiuchumi wananchi wengi liweze kufanikiwa.

Mhe. Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ulipanga kutumia jumla ya TZS 1,027.2 milioni kwa miradi mbali mbali ya wananchi. Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 jumla ya TZS 567.2 milioni zimetolewa. Kati ya fedha hizo, TZS 30 milioni zilitolewa na Serikali na TZS 537.2 milioni ni mchango wa Washirika wa Maendeleo. Fedha hizo zimetumika kugharamia utekelezaji wa miradi 77, kati ya hiyo 51 ipo Unguja na 26 Pemba. Mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa miradi yalitolewa nchini kote kwa kamati za miradi iliyopatiwa fedha.

Miradi ya Wananchi

Mhe. Spika, Serikali pia imeendelea kusaidia nguvu za wananchi kupitia miradi midogo midogo waliyoiibua na kuiendeleza wenyewe. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 miongoni mwa miradi iliyofaidika ni ya elimu, afya, usambazaji maji, usambazaji umeme, kilimo na matengenezo madogo madogo ya barabara. Jumla ya TZS 500 milioni zilitengwa kwa mwaka 2009/2010 na hadi Machi 2010, matumizi yamefikia TZS 162.3 milioni sawa na asilimia 32.5 ya lengo la mwaka. Kukatika kwa umeme katika kipindi hicho kumepunguza kasi ya kufanya ziara na tathmini ya miradi na hivyo kuwepo kwa idadi ndogo ya maombi yaliyoweza kushughulikiwa.

Utamaduni na Michezo

Mhe. Spika, katika kuendeleza na kuhifadhi kumbukumbu za kihistoria na mambo ya kale, Magofu ya Mkoani, Vitongoji, Pujini, Mkamandume, Bihole, Maruhubi na Kuumbi yanaendelea kufanyiwa matengenezo. Mkandarasi

amepatikana kwa ajili ya kuandaa michoro kwa matengenezo ya majengo ya Beit-el-Ajab na Makumbusho ya Mnazi Mmoja. Aidha, kazi ya kuweka alama na vielelezo katika maeneo ya kale inaendelea na maeneo 40 (27 Unguja na 13 Pemba) tayari yamepimwa.

Mhe. Spika, katika mradi wa kujenga uwezo wa Taasisi ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe, Sheria ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe ya mwaka 1994 imefutwa na kutungwa mpya.

Mhe. Spika, Sekta ya Utamaduni imeanza kazi za kuweka ramani ya utamaduni na hivi karibuni chapisho la ramani hiyo litatoka. Kwa upande wa Sekta ya Michezo, Mradi wa Matengenezo ya Uwanja wa Amaan umekamilika. Miongoni mwa matengenezo makubwa yaliyofanywa ni pamoja na kuweka paa jipya na la kisasa kwenye sehemu ya *VIP* na Jukwaa la *Orbit*, kujenga upya sehemu ya kuchezea mpira wa miguu *(football pitch)*, kuweka mpira mpya wa kukimbilia pamoja na ujenzi wa sehemu za michezo midogo midogo ya ndani, pia kuweka bao la matokeo la dijitali *(LCD-Score Board)*, uimarishaji wa uzio, barabara ya mzunguko nje ya uwanja, kubadilisha mifumo yote ya maji na umeme, pamoja na kuchimba kisima kipya cha maji na kuweka jenereta la akiba.

Mhe. Spika, kwa upande wa Kiwanja cha Gombani, ufungaji wa umeme mkubwa kwa ajili ya taa umekamilika. Ufungaji wa taa hizo kwenye minara unatarajiwa kufanyika hivi karibuni. Kazi ya uwekaji nyasi bandia kwenye uwanja huo inatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2010.

KLASTA YA UTAWALA BORA NA UMOJA WA KITAIFA

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/10, Klasta ya Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa ina jumla ya programu tano na miradi 16 iliyopangiwa kutumia TZS 13,770 milioni sawa na asilimia 5.7 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, TZS 7,332 milioni ni mchango wa serikali, sawa na asilimia 18 ya mchango wake katika bajeti ya maendeleo. Fedha zilizobakia, TZS 6,438 milioni, ni mchango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 3.2 ya makadirio ya mchango wao kwa bajeti ya maendeleo. Kuanzia Julai 2009 hadi Machi 2010, Klasta hii imetumia jumla ya TZS 9,844 milioni sawa na asilimia 59 ya bajeti yake. Kati ya fedha hizo, Serikali imetoa TZS 5,650 milioni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya mchango wake kwa Klasta hii na Washirika wa Maendeleo wamechangia TZS 4,194 milioni sawa na asilimia 46 ya makadirio ya awali.

Utumishi wa Umma

Mhe. Spika, katika kuimarisha utoaji wa huduma bora na kurekebisha Utumishi wa Umma, wataalamu waliandaa taarifa ya uchambuzi wa hali halisi *(Situation Analysis)* ya Marekebisho ya Utumishi Serikalini. Taarifa hiyo imetumika katika utayarishaji wa Mpango Mkakati wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma – Zanzibar.

Mhe. Spika, Mapitio ya Mfumo wa Ulipaji wa Mishahara *(Review of Payroll System)* yalifanyika na kuainisha maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho ambayo yameingizwa katika Mpango Mkakati wa Utumishi wa Umma. Mkakati huo umeainisha maeneo makuu sita ambayo yametiliwa mkazo wa kutekelezwa katika kipindi cha miaka miwili (2010/2011 – 2011/2012). Maeneo hayo ni: kuimarisha taasisi, miundo na mifumo ya utoaji wa huduma za jamii, kuimarisha Utumishi wa Umma, kuimarisha Serikali za Mitaa, utunzaji kumbukumbu na taarifa, usimamizi na uwajibikaji wa Programu hiyo. Uandaaji wa Programu hiyo umefaidika na msaada kutoka Benki ya Dunia.

Mhe. Spika, Rasimu ya Awali ya Sera ya Utumishi Serikalini inaendelea kufanyiwa kazi, ambapo wataalamu kwa kushirikiana na kikosi kazi wapo katika hatua za mwisho za utayarishaji wa Sera hiyo. Aidha, Kamati ya Kutayarisha Sheria ya Utumishi wa Umma imewasilisha muundo wa Rasimu ya Sheria hiyo ambao umepitiwa na wataalamu wa Serikali kwa kupatiwa michango na miongozo ili kuweza kukamilisha rasimu ya awali.

Mhe. Spika, katika kuimarisha utawala wa Sheria, upatikanaji wa nakla za kutosha za Sheria mbali mbali ni suala muhimu. Jumla ya Juzuu *(volumes)* 14 za nakala za Sheria za Zanzibar za mwaka 1980 hadi 2008 zimechapishwa na kusambazwa kwa watumiaji Serikalini, taasisi za sheria, Maktaba Kuu, Vyuo vya Elimu na kwa Wanasheria. Vile vile matangazo 20 ya sheria yalitayarishwa na miswada minane ya sheria iliandikwa na kuwasilishwa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Mhe. Spika, juhudi za kuiimarisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka zimeendelezwa kwa kuimarisha sheria ya kuanzishwa kwake na kuimarisha mazingira ya kazi kwa kuzindua jengo lake jipya. Mbali ya ofisi, jengo hilo lina maktaba ya kisasa yenye kutoa habari kwa kutumia teknolojia ya kisasa *(Multi Media Room)* na mtambo maalum wa mawasiliano *(video conference).* Huduma hii itawawezesha watumiaji kufuatilia na kushiriki mijadala na mikutano ya kitaifa na kimataifa wakiwa hapa Zanzibar pamoja na kutumika kama kielelezo cha ushahidi kwa shahidi aliye nje ya Zanzibar. Mipango ya ujenzi wa Ofisi Pemba inaendelea ambapo tayari kiwanja kimepatikana hapo

Tibirinzi, Chake Chake. Mshauri wa ujenzi ameshakamilisha michoro kwa ajili ya ujenzi huo.

Vizazi na Vifo

Mhe. Spika, taarifa za vizazi na vifo ni muhimu sana kwa mipango ya nchi. Ili kuweza kuimarisha ukusanyaji wake, Serikali imewapatia Wasaidizi Warajis wa Wilaya zote za Pemba na Unguja mafunzo ya uingizaji taarifa hizo katika kompyuta. Aidha, Wilaya zote zimepatiwa kompyuta kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Mhe. Spika, sambamba na lengo la MKUZA la kuweka mazingira bora ya kazi, ujenzi wa jengo jipya la Baraza la Wawakilishi Mbweni umo katika hatua za mwisho. Aidha, ujenzi wa Hospitali ya KMKM - KIBWENI unaendelea kwa kazi za ujenzi wa kitengo cha mama wajawazito na watoto, ushauri nasaha *(HIV/AIDS)* na duka la dawa. Ukarabati wa jengo la Mahkama Kuu Vuga umeanza kwa matengenezo ya uezekaji wa paa na kutandika dari. Kwa upande wa Mahkama ya Tunguu, ujenzi umeanza kwa kujenga uzio. Ujenzi wa jengo la Mrajis Pemba umekamilika na Ofisi mbali mbali katika jengo la Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora zimefanyiwa ukarabati. Taratibu za ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Unguja na Pemba zimeanza kwa kupata viwanja na kuanza hatua za awali.

Mhe. Spika, kazi za ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Kazi, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto (Pemba) inatarajiwa kuanza hivi karibuni kwa vile kiwanja tayari kimeshapatikana. Hatua za matayarisho zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji (Pemba). Katika ukamilishaji wa ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Unguja, kazi ya ujenzi wa ghala na uzio umekamilika.

Mhe. Spika, maeneo mengine yaliyoendelea kuimarishwa ni pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, masuala ya ununuzi, usimamizi na uondoaji wa mali za Serikali na mashirikiano na sekta binafsi. Aidha, ushirikiano na Sekta binafsi katika juhudi za kuleta maendeleo kupitia Baraza la Biashara *(ZBC)* unaendelea kwa mafanikio kama nilivyosema hapo awali.

Mhe. Spika, katika kuendeleza uhuru wa kupata habari kwa wananchi, serikali imeendeleza utamaduni wa kuvipa uhuru vyombo vya habari. Kwa upande wa vyombo vya Serikali, Gazeti la Zanzibar Leo limeimarishwa. Shirika jipya la Magazeti ya Serikali limeundwa. Aidha, Sauti ya Tanzania Zanzibar imeimarishwa kwa kufungiwa mtambo mpya wa masafa ya kati wenye nguvu za KW 100 na vifaa vyake, kupitia msaada kutoka Jamhuri ya Watu wa

China. Vile vile *antenna* mbili zimefungwa katika kituo cha TVZ huko Pemba ambazo zitasaidia kuondoa tatizo la urushaji wa matangazo.

Takwimu

Mhe. Spika, ukusanyaji na uimarishaji wa takwimu sahihi ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kazi mbali mbali zimeendelea kutekelezwa kwa mwaka unaoendelea wa 2009/10. Miongoni mwa kazi hizo ni Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya, Sensa ya Kilimo, Sensa ya Uzalishaji Viwandani, Utafiti wa Hali ya Chakula, Utafiti wa Hali ya Afya, Mama na Mtoto, na Utafiti wa Viashiria vya Uchumi Tanzania. Aidha, matayarisho kwa Utafiti wa Hali ya Nguvukazi na Ajira unaosimamiwa na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na ile ya Sensa ya Watu iliyopangwa kufanyika mwaka 2012 yameendelea.

Mhe. Spika, Serikali imeendelea kuheshimu haki za binaadamu zikiwemo za uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kujiunga pamoja *(freedom of association)*, na uhuru wa kuabudu, miongoni mwa nyengine. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuridhia kuwa Tume ya Haki za Binaadamu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifanye kazi zake mpaka Zanzibar. Serikali ilifanyia mapitio Sheria za Makosa ya Jinai za mwaka 2000, Sheria Namba 3 na 4 ya mwaka 1995 na Sheria Namba 1 ya mwaka 1998 kwa lengo la kuimarisha mahusiano kati ya Serikali na jamii.

Mhe. Spika, nchi yetu imekabiliwa na Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba mwaka huu ambao utaweka madarakani awamu mpya ya Serikali. Maandalizi ya uchaguzi huo yanaendelea vyema kuhakikisha kuwa kila mwenye haki ya kupiga kura anafanya hivyo na uchaguzi huo unakuwa wa haki na huru. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imefanya mapitio ya fomu za uchaguzi ambazo zinahusisha uteuzi wa wagombea, upigaji picha na kuhesabu kura. Aidha, kanuni mbali mbali zitakazotumika wakati wa uchaguzi zimeandaliwa ikiwemo: Kanuni ya Uchaguzi, Kanuni ya Ukaguzi wa Daftari, Kanuni kwa Washiriki wa Uchaguzi na Kanuni kwa Waangalizi wa Uchaguzi.

Mhe. Spika, kazi ya uandikishaji wapiga kura katika daftari la kudumu imefanyika kwa awamu mbili ili kumpa fursa kila mwananchi aliyetimiza sifa za uandikishaji kupata haki hiyo. Vile vile, mkutano wa Asasi za Kiraia umeandaliwa kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika utoaji wa elimu ya wapiga kura.

MASUALA MTAMBUKA

Mhe. Spika, masuala ya idadi ya watu, utawala bora, VVU/UKIMWI na mazingira ni miongoni mwa masuala mtambuka ambayo yanastahiki kupewa umuhimu katika utayarishaji wa sera na mipango ya utekelezaji.

Mhe. Spika, katika masuala ya idadi ya watu, mkazo ulikuwa ni kuingiza viashiria vyake katika mchakato wa utayarishaji wa mipango na bajeti, yakiwemo masuala ya jinsia. Katika kipindi hiki mambo yafuatayo yametekelezwa:-

Kukamilika mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Idadi ya Watu, kuwajengea uwezo watendaji wakuu katika uzalishaji wa takwimu na uchambuzi wake, kutoa mafunzo yanayohusiana na uingizaji wa masuala ya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo na bajeti ikiwemo upunguzaji wa umasikini. Vile vile, wadau mbali mbali katika ngazi zote (wilaya, mikoa, wizara, idara na taasisi mbali mbali pamoja na watunga sera na watoa maamuzi) walijengewa uwezo juu ya umuhimu wa kuingiza masuala ya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo na bajeti.

Mhe. Spika, Serikali inatambua kuwa wanawake wanaunda sehemu kubwa na muhimu ya jamii yetu. Ushiriki wa wanawake katika mipango ya maendeleo na utekelezaji wake ni muhimu sana. Pamoja na juhudi za uwezeshaji nilizozieleza hapo kabla, Zanzibar imeendeleza mafanikio yaliyopatikana katika nyanja ya elimu ambapo kuna usawa. Katika nafasi za sera na maamuzi, hadi sasa kuna wanawake 29 kati ya jumla ya nafasi 133 zilizopo zikihusisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Mawaziri, Naibu Waziri, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Makatibu Wakuu na Manaibu wao. Serikali imekusudia kuongeza nafasi za wanawake katika Baraza la Wawakilishi kutoka asilimia 25 ya Wajumbe wa kuchaguliwa iliyopo sasa hadi asilimia 40.

Mhe. Spika, utafiti wa viashiria vya UKIMWI na Malaria kwa mwaka 2008 umeonyesha kwamba kiwango cha maambukizi ya ukimwi ni asilimia 0.6. ukiathiri zaidi rika la kati ya miaka 15 – 49. Hata hivyo, utafiti mwengine umeonesha kuwa UKIMWI upo zaidi kwa makundi maalum kama ya watumiaji wa dawa za kulevya, watu wanaojihusisha na biashara ya ngono, na wale wanaojihusisha na ngono ya jinsia moja. Pamoja na asilimia ndogo ya maambukizi hayo ikilinganishwa na nchi za jirani, tahadhari zaidi inahitajika kuhakikisha kwamba maradhi haya hayaenei zaidi. Serikali ilichukuwa jitihada kubwa zaidi katika kuelimisha jamii na makundi yaliyo katika hatari zaidi juu ya masuala ya VVU na maradhi ya UKIMWI.

Mhe. Spika, maendeleo endelevu ni yale yanayozingatia, miongoni mwa mambo mengine, utunzaji wa mazingira kwa faida ya kizazi kilichopo na vijavyo. Umaskini unaombatana na kukuwa kwa idadi ya watu nao unachangia katika uharibifu wa mazingira kutokana na muingiliano mkubwa zaidi baina ya watu na mazingira yanayowazunguka kwa sababu za kiuchumi na kijamii. Matumizi makubwa kwa ajili ya kuni na miti ya kujengea, njia duni za uvuvi, uchimbaji wa mawe na matumizi mengine yanayoharibu ardhi ni mifano ya uharibifu unaotokana na umaskini na ongezeko la idadi ya watu.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, nchi yetu, kama ilivyo kwa dunia nzima, ina changamoto ya kukabiliana na athari ya mabadiliko yanayoendelea ya hali ya hewa duniani. Kwa kuwa nchi yetu ni visiwa, mazingira ya ukanda wa Pwani yana umuhimu wa pekee kiuchumi na kijamii. Katika uhifadhi wake, kazi ya utayarishaji wa Mkakati wa Mpango wa Uwiano wa Ukanda wa Pwani imekamilika. Aidha, utafiti ulifanyika katika maeneo yaliyoathirika na mmong'onyoko wa fukwe ikiwemo Jambiani, Nungwi, Kisiwa Panza, Tumbe na Micheweni. Matokeo ya utafiti huo yatasaidia katika kuamua hatua za kuchukuliwa. Kufanikiwa kwa juhudi za kupunguza umaskini kupitia utekelezaji wa MKUZA kunatarajiwa pia kusaidia kupunguza athari za mazingira. Serikali inaendelea kushirikiana na jumuiya za kimataifa katika kutathmini na kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa duniani.

Mhe. Spika, katika utunzaji wa mazingira na kupambana na umasikini, serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira yaani *Sustainable Management of Land and Environment – (SMOLE)* na Programu ya Uhifadhi wa Mazingira ya Bahari (*MACEMP*). Chini ya Programu ya MACEMP, jumla ya miradi 48 yenye thamani ya Tsh 779.7 milioni ilipatiwa fedha kupitia *MACEMP*/*TASAF*. Kati ya miradi hiyo, 22 yenye thamani ya TZS 410.0 milioni imetekelezwa Unguja na miradi 26 yenye thamani ya TZS 369.7 milioni imetekelezwa Pemba katika kipindi cha 2009/2010. Vile vile serikali imefanya mapitio ya miradi ya vitega uchumi kwa ajili ya kutathmini athari za kimazingira zinazoweza kutokea na imeelimisha wananchi juu ya hifadhi ya misitu na namna ya ufugaji bora wa nyuki.

UTEKELEZAJI WA BAJETI 2009/10

Mapato ya Serikali Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/10, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya TZS 412,605 milioni ambapo kati ya hizo TZS 159,697 milioni ni mapato ya ndani, TZS 50,214 milioni ni misaada ya kibajeti, na TZS 199,188 milioni ni ruzuku na mikopo kwa programu na miradi ya maendeleo. Mapato halisi hadi Machi 2010 yamefikia TZS 247,761 milioni, sawa na asilimia 60.0 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Spika, kwa miezi tisa hadi Machi 2010, taasisi za ukusanyaji za *TRA* na *ZRB* ziliweza kukusanya mapato ya ndani ya TZS 113,918 milioni sawa na asilimia 71.3 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji huo unaonesha ongezeko la mapato ya TZS 10,685.5 milioni sawa na ukuaji wa asilimia 10.4 ikilinganishwa na kipindi cha miezi tisa katika mwaka 2008/09 ambapo TZS 103,233 milioni zilikusanywa kutokana na mapato ya ndani. Matarajio ya makusanyo hadi Juni 2010 ni kufikia TZS 146,169 milioni sawa na asilimia 91.5 ya lengo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/10 Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA*, ilitarajiwa kukusanya TZS 63,235 milioni sawa na asilimia 39.6 ya mapato yote ya ndani. Hadi Machi 2010 *TRA* ilikusanya TZS 43,803 milioni sawa na asilimia 69.3 ya lengo la mwaka. Kati ya makusanyo hayo Idara ya Forodha imekusanya TZS 26,189 milioni sawa na asilimia 67.4 ya lengo lake la mwaka wakati Idara ya Kodi za ndani imekusanya TZS 17,614 milioni sawa na asilimia 72.2 ya lengo la mwaka. Mchango halisi wa mapato ya *TRA* umefikia asilimia 38.5 ya mapato yote ya ndani ukiwa ni pungufu kidogo kulinganisha na matarajio ya awali ya kuchangia asilimia 39.6.

Mhe. Spika, kati ya mapato yaliyokusanya na TRA, makusanyo ya ushuru wa forodha yalifikia TZS 10,741 milioni sawa na asilimia 69.1 ya lengo la mwaka. Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutokana na uagiziaji ilifikia TZS 10,047 milioni ya makadirio ya mwaka. Mapato mengine yanayokusanywa na Idara ya Forodha yalifikia TZS 5,401 milioni. Kwa ujumla, mapato yatokanayo na forodha yameongezeka kwa asilimia 5.7 kutoka TZS 24,781 milioni katika miezi tisa ya mwaka 2008/09 hadi TZS 26,189 milioni katika kipindi kama hicho mwaka 2009/10.

Mhe. Spika, kwa upande wa makusanyo yatokanayo na kodi ya mapato, TZS 8,566 milioni sawa na asilimia 74.3 zilikusanywa kutokana na mapato yatokanayo na ajira (*PAYE*). Kodi kutokana na watu binafsi na mashirika ilifikia TZS 6,038 milioni sawa na asilimia 66.9 ya makadirio ya mwaka. Mapato mengine yaliyokusanywa na Idara ya Kodi za Ndani yalifikia TZS 3,010 milioni. Kwa ujumla, mapato yatokanayo na Kodi ya Mapato yameongezeka kwa asilimia 20.4 ikilinganishwa na kipindi cha miezi tisa kwa mwaka 2008/09 kutoka TZS 14,634 milioni katika mwaka 2008/09 hadi TZS 17,614 milioni katika mwaka 2009/10. Kuimarika kwa hatua za ufuatiliaji, uhakiki, ukaguzi na ugomboaji wa madeni ya kodi kumesaidia katika kuongeza uwajibikaji na ukuaji wa mapato.

Mhe. Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar *ZRB* kwa mwaka 2009/10 ilipangiwa kukusanya TZS 85,773 milioni sawa na asilimia 60.4 ya mapato yote ya ndani kabla ya kuzingatia mapato yatokanayo na mawizara. Hadi kufikia mwezi

Machi 2010, *ZRB* ilikusanya TZS 64,259 milioni sawa na asilimia 74.9 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji huo unaonesha ongezeko la mapato la TZS 13,119 milioni sawa na asilimia 23.0 ikilinganishwa na kipindi cha miezi tisa katika mwaka 2008/09 ambapo TZS 56,996 milioni zilikusanywa kutokana na mapato ya ndani.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa, mapato yatokanayo na Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) yamefikia jumla ya TZS 27,664 milioni sawa na asilimia 80 ya makadirio ya mwaka. Kodi ya ushuru wa bidhaa imefikia TZS 5,799 milioni sawa na asilimia 128.8 ya makadirio ya mwaka. Aidha, *ZRB* ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS 28,674 milioni kutokana na ushuru wa mahoteli, ushuru wa watembeza wageni, ushuru wa mikahawa, ushuru wa stempu, ushuru wa petroli, usajili wa magari, leseni za udereva na magari, ada ya viwanja vya ndege na bandari, mfuko wa kuendeleza barabara pamoja na ada ya usalama wa viwanja vya ndege. Utekelezaji halisi umefikia TZS 30,796 milioni sawa na asilimia 107.4 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Spika, mapato yasiyokuwa ya kodi kwa mwaka 2009/10 yalikadiriwa kufikia TZS 10,765 milioni. Makusanyo halisi kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2009/10 yalifikia TZS 5,856 milioni sawa na asilimia 54.4 ya makadirio ya mwaka. Matarajio ya vyanzo visivyokuwa vya kodi hadi Juni 2010 ni kufikia TZS 8,369 milioni sawa na asilimia 77.7 ya lengo la mwaka. Kwa ujumla, matarajio ya makusanyo kwa *ZRB* hadi Juni 2010 ni kufikia TZS 80,391 milioni sawa na asilimia 93.7 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Spika, mbali na mapato yatokanayo na vianzio vya ndani, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kama ilivyo kwa nchi nyingi zinazoendelea, hupokea misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia misaada ya kibajeti au ruzuku na mikopo kwa kazi za maendeleo. Kwa mwaka wa 2009/10 Serikali ilitarajia kupokea mapato yanayotokana na misaada ya kibajeti (*GBS* - 4.5%) yenye jumla ya TZS 50,214 milioni. Hadi kufikia Machi 2010, jumla ya TZS 40,926 milioni zimepatikana sawa na asilimia 81.5 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Spika, fedha za mikopo na ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zilikadiriwa kufikia TZS 199,188 milioni kwa mwaka 2009/10 ambapo ruzuku ni TZS 96,879 milioni na mikopo ni TZS 102,309 milioni. Hadi kufikia mwezi Machi 2010 fedha zilizopokelewa ni TZS 92,917 milioni. Fedha hizo ni sawa na asilimia 46.4 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo TZS 65,456 milioni ni Ruzuku na TZS 27,461 milioni ni Mikopo.

Mhe. Spika, orodha ya nchi, mashirika ya kimataifa na watu binafsi waliochangia katika bajeti hiyo ni kubwa na isingekuwa busara kuisoma yote hapa. Naomba itoshe kwa washirika wote kupokea shukrani zangu kwao kwa

pamoja na kila mmoja kati yao. SMZ na wananchi wa Zanzibar tunathamini na kushukuru sana misaada hii ambayo ni chachu ya maendeleo yetu.

MATUMIZI

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/10 Serikali ilipanga kutumia jumla ya TZS 412,605 milioni sawa na asilimia 47 ya Pato la Taifa. Kati ya hizo, TZS 172,692 milioni ni kwa matumizi ya kawaida. Katika kipindi cha miezi tisa TZS 114,475 milioni zilitumika kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 66.3 ya makadirio ya mwaka. Kati ya matumizi hayo TZS 52,164 milioni sawa na asilimia 70.7 ya makadirio ya mwaka ya kasma hiyo zimetumika kwa ajili ya mishahara. Ruzuku kwa taasisi mbalimbali imefikia TZS 15,532 milioni sawa na asilimia 73.3 ya lengo la mwaka wakati matumizi mengineyo ni TZS 25,304 milioni sawa na asilimia 64.9 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Spika, serikali kwa mwaka 2009/10 ilipanga kutumia jumla ya TZS 239,913 milioni kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, TZS 40,725 milioni ni mchango wa serikali na Tsh 199,188 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2010, matumizi halisi kwa fedha za ndani yamefikia TZS 28,291 milioni sawa na asilimia 69.5 ya makadirio ya mwaka. Matumizi halisi ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya programu na miradi yamefikia TZS 66,986 milioni sawa na asilimia 32 ya makadirio ya mwaka. Jumla ya TZS 92,917 milioni zimetolewa na Washirika wa Maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 46.4 ya makadirio ya mwaka.

UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO

Mhe. Spika, hatua mbalimbali zilizopangwa kutekelezwa na Serikali kwa ajili ya kuimarisha mapato kwa mwaka 2009/10 zimetekelezwa kwa viwango tofauti. Serikali imepunguza kiwango cha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka asilimia 20 hadi 18 kama ilivyokubaliwa katika mapendekezo ya bajeti ya 2009/10 kwa dhamira ya kupunguza athari za msukosuko wa fedha duniani na kuendelea kushajiisha uzalishaji. Mamlaka ya Mapato (*TRA*) na Bodi ya Mapato (*ZRB*) tayari zimeanzisha utaratibu wa vikao vya Baraza la Walipakodi. Nia ni kuleta mahusiano mazuri na ya karibu baina ya walipa na wakusanya kodi ili kuimarisha uwajibikaji wa hiari na kutatua kwa wakati kero zinazowakabili walipakodi.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na vianzio vya kodi na taratibu zake, Bodi ya Mapato Zanzibar imeimarisha Mfumo wa Taasisi kwa kuanzisha “Idara ya Mapato ya Mawizara” kwa lengo

la kusimamia mapato hayo. Awali jukumu hilo likisimamiwa na Kitengo cha Mapato ya Mawizara chini ya "Idara ya Kodi Nyenginezo**"**. *ZRB* pia imekamilisha mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji ulio bora na rahisi unaotumia mtandao wa kompyuta katika kutambua walipakodi, malipo na madeni kwa kuanzia na ya kodi ya ardhi.

Mhe. Spika, utozaji wa kodi ya ardhi kwenye matumizi ya bahari yanayoambatana na ujenzi wa gati (*Jetty*) katika hoteli za kitalii ulianza rasmi Julai 2009. Ukusanyaji utafanyika sambamba na malipo ya walipakodi husika kila mwaka.

Mhe. Spika, matayarisho ya uandaaji wa sera ya kodi nchini yameendelea. Hata hivyo, uandaaji huo unaambatana na mambo kadhaa ambayo yanalazimika kukamilika kwanza kabla ya kuandaa sera yenyewe. Mwelekeo ni kuandaa sera inayozingatia upeo mzima wa usimamizi wa kodi nchini ikiwemo za serikali za mitaa. Hatua zilizofanyika ni pamoja na matayarisho ya Mageuzi ya serikali za Mitaa chini ya Mageuzi ya sekta ya Umma ambayo yatahusisha pia mageuzi katika usimamizi wa mapato ya serikali za mitaa. Utafiti pia umefanyika kuangalia uwezekano wa kodi za ndani za Muungano kusimamiwa na *ZRB*. Serikali itajadiliana na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kukubaliana na hatua zinazofuata ili kuepusha athari za mapato na watumishi wataohusika. Utafiti pia unafanyika katika utozaji kodi katika sekta isiyo rasmi na unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni 2010. Mambo yote haya ni muhimu ili kuandaa Sera bora ya Kodi kwa Zanzibar.

UTAYARISHAJI WA MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASIKINI ZANZIBAR (MKUZA II)

Mhe. Spika, muda wa utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA), kama Mkakati wa muda wa kati wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2020 unakamilika mwezi Juni 2010 baada ya kuzinduliwa Machi mwaka 2007 kwa kutekelezwa kwa miaka mitatu. Ripoti za kila mwaka za ufuatiliaji wa utekelezaji wa MKUZA (*MKUZA Annual Implementation Report*) zimeandaliwa kwa miaka 2007/2008 na 2008/2009 kuangalia mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizokabili katika vipindi hivyo, na hatua zilizohitajika kurekebisha kasoro zilizojitokeza.

Mhe. Spika, sura nzuri zaidi ya hali ya umaskini itajulikana baada ya kukamilika taarifa ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (*Household Budget Survey*) uliofanyika mwaka huu wa 2009/10. Hata hivyo, Ripoti ya Maendeleo ya Watu Zanzibar (*Zanzibar Human Development Report*)

ilitayarishwa kwa mara ya kwanza hapa Zanzibar mwaka 2009. Ripoti kama hizi zimekuwa zikitolewa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa kwa nchi zote duniani, ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tokea mwaka 1990. Lengo la Ripoti hizo ni kupima maendeleo kwa upeo mpana zaidi kuliko kutumia kigezo cha ukuaji wa uchumi pekee. Ripoti ya Zanzibar imeonesha kuwa kimsingi Zanzibar haitofautiani na nchi nyengine zinazoendelea kusini mwa Jangwa la Sahara. Hata hivyo, imeonesha pia mafanikio katika maendeleo ya elimu, hali ya afya, utawala bora na maeneo mtambuka.

Mhe. Spika, Serikali imeendelea na mapitio ya MKUZA na uandaaji wa Mkakati mpya wa miaka mitano 2010 – 2015. Jumla ya tafiti 17 zilmefanywa. Matokeo ya tafiti hizo yametumiwa katika utayarishaji wa MKUZA II sambamba na mafunzo yaliotokana na utekelezaji wa MKUZA kwa miaka 2007 - 2010. Rasimu ya mwanzo ya MKUZA II imekamilika tayari kwa kujadiliwa na wadau mbali mbali Unguja na Pemba na hatimae kuidhinishwa.

UHUSIANO WA KIFEDHA NDANI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Mhe. Spika, wakati wa kuwasilisha hotuba yangu ya Wizara ya Fedha na Uchumi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2008/2009, nilitoa maelezo ya hatua zilizofikiwa katika uhusiano wa kifedha ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maeneo ya mgao kutokana na misaada ya kibajeti, gawio kutokana na faida ya Benki Kuu, hisa za Zanzibar kutokana na iliyokuwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki (*EACB*) pamoja na utafutaji wa mikopo kutoka nje ya nchi. Aidha nilitoa taarifa kuwa Serikali zetu mbili zilikwisha pokea mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha juu ya uhusiano wa kifedha baina ya SMT na SMZ kuhusiana na mgao na mchango wa kila upande katika mapato na gharama za muungano. Mapendekezo hayo ya Tume yanaendana na matakwa ya vifungu vya 133 na 134 vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 na kifungu cha 115 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Spika, katika majadiliano ya mikutano ya Kamati ya kutatua Kero za Muungano inayoongozwa na Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein, Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwashirikisha Waziri Kiongozi wa SMZ na Waziri Mkuu wa SMT, mambo hayo yote, isipokuwa la mapendekezo ya Tume ya Pamoja, yamekuwa yakijadiliwa. Masuala mengine ya uhusiano ya kifedha yaliyojadiliwa katika Kamati hiyo ni pamoja na malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili wanapohamisha bidhaa kupeleka Tanzania Bara, Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa Muungano waliopo Zanzibar kutohamishiwa Zanzibar

na kutotambuliwa namba za usajili wa vyombo vya moto vya Zanzibar pindi vinapohamishiwa Tanzania Bara.

Mhe. Spika, mafanikio yamepatikana kwa kuyapatia ufumbuzi maeneo sita kati ya hayo tisa, wakati bado majadiliano yanaendelea katika masuala mengine mawili. Aidha majadiliano katika eneo moja bado hayajaanza.

a) Ugawaji wa mikopo ya kibajeti (*General Budget Support Credit*).

Tokea mwaka 2003/2004 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipata mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya kugharamia juhudi za kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Zanzibar haikuwa ikinufaika na mikopo hiyo na hivyo suala hili kuwasilishwa ili kupatiwa ufumbuzi. Kupitia Kamati ya kutatua Kero za Muungano, makubaliano yamefikiwa kuwa Zanzibar nayo ina haki ya kunufaika na mikopo hiyo. SMZ tayari imeanza kunufaika na mikopo ya misaada ya kibajeti (4.5%) kuanzia mwaka 2009/2010. Aidha, imekubalika kuwa SMZ ishirikishwe katika mchakato mzima wa utafutaji misaada ya kibajeti ili kusaidia vyema utekelezaji wa MKUZA. Ili kuwa na utaratibu bayana wa mikopo kwa mambo ambayo si ya Muungano, Kamati ndogo ya watu wanne imeundwa kushughulikia utaratibu wa mikopo ya aina hiyo.

b) Mgawanyo wa fedha zitokanazo na misamaha ya madeni (MDRI).

Suala hili liliwasilishwa kutokana na ucheleweshaji mkubwa kwa SMZ nayo kunufaika na fedha hizo. SMZ imeshapata fedha za misamaha hiyo (MDRI) hivyo suala hili nalo limetatuliwa.

c) Uwezo wa SMZ kukopa ndani na nje ya nchi

Kimsingi suala hili limepatiwa ufumbuzi, na SMZ tayari inakopa kupitia *BOT* na Wizara ya Fedha na Uchumi SMT. Wizara za Fedha na Uchumi SMT na SMZ zimetakiwa kuandaa utaratibu mzuri utakaondowa urasimu katika SMZ kupata mikopo ya nje.

d) Malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili.

Hili ni lalamiko la muda mrefu kwa wafanyabiashara wa Zanzibar. Kwa sasa imekubaliwa kwamba bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha taratibu zote za kiforodha kupitia kituo chochote rasmi cha forodha zitahesabika kuwa zimeingizwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, katika kuhakikisha tatizo hili halijitokezi tena, Mamlaka ya Mapato Tanzania itachukua hatua za kinidhamu kwa watendaji wanaotumia vibaya fursa ya ukadiriaji wa thamani za bidhaa.

e) Kodi ya Mapato

Imekubaliwa kuwa kodi ya mapato inayotokana na mishahara, sheria irekebishwe ili mapato hayo yaweze kuwasilishwa sehemu ambayo watumishi wanapofanyia kazi. Aidha kodi ya mapato inayozuiwa (*withholding tax*), sheria irekebishwe ili mapato yanayokusanywa na kampuni au mashirika kwa upande wa SMZ yabaki Zanzibar na yale yanayokusanywa SMT yabaki Tanzania Bara.

f) Usajili wa Magari

Imekubaliwa kuwa, gari iliyosajiliwa upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupelekwa upande mwengine ijulikane kuwa imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, sheria zote zinazohitajika kufanyiwa marekebisho kutoka pande mbili za Muungano zirekebishwe na kuimarisha "*Data Base*" inayojumuisha habari zote zinazohusu usajili wa magari.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza, bado yapo mambo ambayo hayajapatiwa ufumbuzi na majadiliano yanaendelea. Mambo hayo ni:

(a) Gawio la Faida ya Benki Kuu na

(b) Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, SMZ inaamini kuwa inastahili kiwango cha juu zaidi kuliko cha asilimia 4.5 inachopata sasa katika mgao wa gawio kutokana na faida ya BOT. Mtazamo huu unatokana na mchango wake kutokana na fedha zilizotoka kwa iliyokuwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki wakati wa kuanzishwa Benki Kuu.

Suala hili linaungana pia na suala la hisa za SMZ katika iliyokuwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki.

Kazi ya kupitia kumbukumbu inaendelea na taarifa inatarajiwa kuwasilishwa kwa Viongozi wetu Wakuu wa Kero za Muungano, kwanzia Mwenyekiti ambaye ni Makamo wa Rais, Mhe. Waziri Kiongozi wa Zanzibar pamoja na Mhe. Waziri Mkuu si zaidi ya tarehe 24 Juni 2010.

Mhe. Spika, eneo ambalo hadi sasa majadiliano hayajaanza ni kuhusiana na mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha juu ya uhusiano wa kifedha baina ya SMT na SMZ, kuhusiana na mgao na mchango wa kila upande katika mapato na gharama za Muungano. Kwa bahati mbaya hadi sasa upande wa SMT haujawa tayari kwa mazungumzo, ingawa taarifa iliyotolewa ni kuwa mapendekezo hayo yapo katika ngazi ya Baraza la Mawaziri.

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI, MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI 2010/2011

Mwelekeo wa Hali ya Uchumi

Mhe. Spika, Hali ya Uchumi kwa mwaka 2010 inatarajiwa kuimarika zaidi. Utekelezaji wa malengo ya uchumi utakwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA) awamu ya pili, Malengo ya Milenia ya 2015 pamoja na Mageuzi ya Msingi.

Kwa mwaka 2010 pato la taifa linatarajiwa kukua kutoka asilimia 6.7 mwaka 2009 hadi asilimia 7.3 mwaka 2010. Pia kiwango cha mfumko wa bei kinatarajiwa kushuka hadi kufikia asilimia 7.8 mwaka 2010. Mafanikio haya yanategemea kuendeleza zaidi uwekezaji rasilimali, Utekelezaji wa Mkakati wa Ukuzaji Uchumi, Mkakati wa Usafirishaji utakaosaidia na utekelezaji wa juhudi za mageuzi katika sekta ya kilimo, ambayo inatilia mkazo zaidi kuongeza thamani ya bidhaa na kuimarisha biashara ndogo ndogo na za kati (*Micro, Small and Medium Enteprises*).

Matarajio ya kukua kwa uchumi kwa mwaka 2010/11 yanatokana na mambo yafuatayo:-

a) Kukamilika kwa mradi wa umeme wa Tanga-Pemba utakaoleta umeme wa uhakika katika kisiwa cha Pemba ambapo utasaidia kushajiisha uwekezaji;

b) Kuendelea kupungua kwa athari ya msukosuko wa uchumi duniani kutasababisha kuongeza wawekezaji wa kigeni na kuongeza idadi ya watalii;

c) Utekelezaji wa program ya mageuzi ya kilimo Zanzibar ambayo yatashajiisha uzalishaji, kuongeza tija na kuhakikisha uhakika wa chakula (food security);

d) Utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi Zanzibar;

e) Utekelezaji wa Mkakati wa Usafirishaji Zanzibar utakaoimarisha ushirikishwaji wa MSMEs na sekta binafsi kwa mtazamo wa kuongeza nafasi za ajira;

f) Kuimarisha utoaji wa huduma katika viwanja vya ndege na bandarini;

g) Washirika wa Maendeleo wataendelea kusaidia juhudi za maendeleo Zanzibar;

h) Kuendelea utekelezaji Mageuzi ya Msingi; na

i) Kuendelea kuimarisha mazingira mazuri ya kijamii na kisiasa.

Mhe. Spika, baada ya kukamilisha mapitio ya Hali ya Uchumi, Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2009/10, naomba sasa uniruhusu niwasilishe Mwelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka ujao wa fedha 2010/11. Kulingana na malengo ya Dira ya 2020, maeneo yafuatayo yataendelea kupewa msisitizo:-

Maendeleo ya Watu

Mhe. Spika, maendeleo yanapaswa kulenga katika mafanikio ya wananchi walio wengi na kuimarisha uwezo wao. Lengo la msingi la serikali ni kuona wananchi wanaishi maisha marefu yaliyo bora, ambayo ni chaguo lao wenyewe. Kwa mustakabali huo, serikali itaendelea kujenga jamii yenye siha kwa kuimarisha lishe bora na kupitia huduma bora za afya na mazingira mazuri ya kuishi ikiwemo makaazi bora. Uwekezaji utaelekezwa pia kuwaendeleza wananchi kwa kuwapatia elimu bora na ujuzi.Ustawi wa Uchumi.

Mhe. Spika, tafauti kubwa ya kipato katika jamii na kukithiri kwa umaskini ni ishara za matatizo ya kijamii. Dira ya Maendeleo 2020, imelenga katika kufuta umasikini uliokithiri na kuwepo kwa uchumi imara unaohimili ushindani wa kimataifa. Kufikia lengo hili, ni lazima kufanya mageuzi ya mfumo wa kiuchumi, kutoka utegemezi wa uchumi wa kilimo cha kale

(*traditional agriculture*) kwenda uchumi unaofungamana baina ya: (i) utalii endelevu, (ii) uanzishaji wa viwanda, na (iii) kilimo cha kisasa.

Suala la kuongeza thamani katika mazao ya kilimo halinabudi kuzingatiwa kwa undani zaidi. Mageuzi haya yanahitaji sekta binafsi zinazohimili ushindani mkubwa ikiwemo biashara ndogo ndogo na za kati (SMEs), miundo mbinu ya kuaminika na sekta ya fedha imara. Mgawanyo wa rasilimali umezingatia malengo haya muhimu ya Dira 2020.

Uimarishaji Utawala Bora na Demokrasia

Mhe. Spika, kuwepo kwa taasisi zinazoaminika na zenye ufanisi ni sharti muhimu katika kupatikana maendeleo endelevu. Kwa uzito huo, ushirikishwaji wananchi katika mchakato wa maendeleo na katika mambo yanayohusiana na ustawi wao ni jambo la lazima.

Serikali, itakamilisha utayarishaji na kuanza kutekeleza Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma, ambapo pamoja na mambo mengine, itahakikisha kwamba Sekta ya Umma inatoa huduma zenye ubora wa hali ya juu na kwamba Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake ya kisheria. Kasi inayoendelea sasa ya uimarishaji wa demokrasia nchini, itaimarishwa zaidi kwa lengo la kuhakikisha kuendelea kuimarika kwa amani, uvumilivu wa kisiasa na umoja miongoni mwa wananchi.

Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (*CDF*)

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2008/2009 niliahidi kwa niaba ya serikali kulifanyia kazi suala la uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, ili kuweza kuongeza nguvu kwa Waheshimiwa Wawakilishi wa kuchaguliwa kuweza kuhudumia zaidi majimbo wanayoyawakilisha.

Suala hili limechukua muda kukamilika kutokana na haja ya kuzingatia mambo mengi muhimu, likiwemo la kuwa na mfuko mmoja tu kila jimbo utakaosimamiwa kwa pamoja na Mheshimiwa Mwakilishi na Mbunge.

Kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Tanzania tayari imeshaanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, ambao usimamizi wake hauhusishi Mheshimiwa Muwakilishi, basi kuanzia mwaka 2010/2011 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nayo itaanzisha mfuko kama huo, ambao utasimamiwa na Mheshimiwa Muwakilishi kwenye jimbo lake *(Makofi)*.

Kwa kuanzia, fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi Midogo Midogo ya Wananchi, zitatumika kwa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Ili kuendesha vyema mfuko huu, serikali inakusudia katika mwaka huu wa fedha wa 2010/2011 kuwasilisha katika Baraza la Wawakilishi Mswaada wa Sheria wa kuanzisha rasmi mfuko huo mapema iwezekanavyo *(Makofi)*.

MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2010/11

Mhe. Spika, Dira ya Maendeleo ya 2020, Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA II), ambao umebeba Malengo ya Milenia ya 2015, utaendelea kutuongoza katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2010/11. Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2010/11, unakusudia kuzingatia maeneo yaliopewa msisitizo kama yalivyoainishwa hapo juu.

Utekelezaji wa mpango wa kuimarisha usalama wa chakula na lishe unaendana na lengo la maendeleo ya watu. Miradi ya kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama, afya ya jamii hasa inayolenga kupunguza vifo vya mama na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano pia inaendana na lengo hilo. Masuala haya na mengine yamepangwa kutekelezwa chini ya Klasta ya pili ya MKUZA.

Kwa upande wa ujenzi wa uchumi imara unaohimili ushindani, serikali itaendeleza juhudi za uwekezaji katika miundo mbinu hasa ya viwanja vya ndege, barabara na huduma za bandari.

Juhudi pia zitaendelezwa katika kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika na kuaminika, kuongeza uwekezaji na uzalishaji katika kilimo, ili kupunguza utegemezi wa uagiziaji kutoka nje na kushajiisha uongezaji wa thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini. Vile vile hatua za kuimarisha uvuvi wa bahari kuu zitaimarishwa. Masuala haya yanajitokeza katika Klasta ya kwanza ya MKUZA.

Mhe. Spika, kwa upande wa masuala ya Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa, yaliyopo chini ya Klasta ya tatu ya MKUZA, kama nilivyosema awali, utekelezaji wa Mpango wa Kuimarisha Sekta ya Umma utaendelezwa sambamba na utekelezaji wa Mipango Mikakati ya Wilaya na uimarishaji wa Demokrasia.

Kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo, jumla ya shilingi 251,204 milioni zimepangwa kugharamia programu 25 na miradi 94 kwa mwaka 2010/2011. Kati ya fedha hizo shilingi 39,490 milioni sawa na asilimia 15.7

zinatarajiwa kutolewa na serikali na shilingi 211,714 milioni sawa na asilimia 84.3 zinatarajiwa kutolewa na wahisani. Kati ya fedha zinazotarajiwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, shilingi 78,922 milioni ni ruzuku na shilingi 132,792 milioni ni mikopo.

Mhe. Spika, Klasta ya Ukuzaji Uchumi na Upunguzaji Umasikini wa Kipato, inatarajiwa kutekeleza programu 14 na miradi 27 ya maendeleo katika kipindi cha mwaka 2010/2011 kwa gharama ya shilingi 114,434 milioni. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 45.6 ya bajeti yote ya maendeleo.

Kati ya fedha hizo, serikali imetenga jumla ya shilingi 16,744 milioni sawa na asilimia 14.6 ya bajeti ya Klasta na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia jumla ya shilingi 97,690 milioni sawa na asilimia 85.4 ya bajeti ya Klasta kwa mwaka 2010/2011.

Katika Klasta ya Huduma na Ustawi wa Jamii jumla ya programu sita na miradi 37 ya maendeleo inatarajiwa kutekelezwa. Programu na miradi hiyo itagharimu shilingi 110,884 milioni sawa na asilimia 44.1 ya bajeti ya maendeleo. Kati ya hizo serikali imetenga jumla ya shilingi 9,480 milioni sawa na asilimia 8.5 na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia jumla ya shilingi 101,404 milioni sawa na asilimia 91.5 ya bajeti ya Klasta hii kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, katika Klasta ya Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa jumla ya programu tano na miradi 30 ya maendeleo inatarajiwa kutekelezwa. Programu na miradi hiyo itagharimu shilingi 25,886 milioni sawa na asilimia 10.3 ya bajeti ya maendeleo.

Kati ya fedha hizo, serikali imetenga jumla ya shilingi 13,266 milioni sawa na asilimia 51.2 ya bajeti ya Klasta na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia jumla ya shilingi 12,620 milioni sawa na asilimia 48.8 ya bajeti ya Klasta ya tatu kwa mwaka 2010/2011.

MWELEKEO WA BAJETI 2010/11

Mhe. Spika, kwa mara ya kwanza katika historia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wananchi watapata fursa ya kuamua mustakbali wa mfumo wa utawala wanaouwafiki. Fursa hiyo itakayojitokeza kwa upande wa Zanzibar itatokana na uamuzi wa Baraza la Wawakilishi wa kuitisha Kura ya Maoni hapa Zanzibar, ili wananchi waamue wenyewe iwapo baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu Zanzibar ifuate mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa badala ya mfumo uliopo sasa *(Makofi)*.

Chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, serikali itaundwa na vyama vyenye uwakilishi kwenye Baraza la Wawakilishi badala ya mfumo wa sasa ambao chama kilichopata wingi wa asilimia za kura ndio kinachounda serikali. Kwa kufuata misingi ya demokrasia, wananchi wenyewe ndiyo watakaoamua aina ya serikali wanayoiwafiki. Nia ni kuwepo kwa mfumo utakaoimarisha umoja na utulivu miongoni mwa wananchi wote wa Zanzibar *(Makofi)*.

Kwa mujibu wa utaratibu wa kikatiba tuliojiwekea, nchi yetu itafanya Uchaguzi Mkuu baadaye mwaka huu. Kwa kuwa Rais ambaye yupo madarakani anamaliza kutumikia vipindi viwili, hivyo kufikia ukomo wa uongozi, tunatarajia kupata kiongozi mpya baada ya kukamilika uchaguzi huo.

Kutokana na hali ya utulivu na maelewano iliyofikiwa nchini, ni matumaini yangu kuwa uchaguzi wa mara hii utakuwa ni kielelezo zaidi cha kupea kwa demokrasia nchini. Vile vile utakuwa huru, maelewano, amani tena bila ya misukosuko. Tunatarajia kuwa Zanzibar itaandika ukurasa mpya katika uimarishaji wa demokrasia nchini *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa upande wa mgao wa rasilimali, katika bajeti ya serikali katika mwaka ujao wa fedha, bado fedha nyingi zitaelekezwa katika matumizi ya maendeleo kuliko matumizi ya kazi za kawaida. Asilimia 56.5 ya bajeti yote itaelekezwa katika programu na miradi ya maendeleo. Fedha hizi zitaendelea kuwekezwa katika miundombinu ya barabara, kiwanja cha ndege, nishati, kilimo, elimu, maji safi na salama, maeneo mengine yenye maslahi kwa wananchi na jamii kwa jumla.

Kutokana na mwelekeo niliioueleza hapo juu nina furaha kulitangazia Baraza lako tukufu kwamba Bajeti ya mwaka 2010/2011 itakuwa ni **"Bajeti ya Demokrasia na Maendeleo"** *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sio Chama cha Siasa cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ni Bajeti ya Demokrasia na Maendeleao)

MAPATO

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa mwaka ujao wa 2010/11, serikali inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 444,637 milioni, ambapo mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia shilingi 171,687 milioni, wakati yale ya nje ni shilingi 266,950 milioni ambayo yatatokana na misaada ya kibajeti, ruzuku na mikopo kwa program na miradi ya maendeleo.

Mapato ya Ndani

Mhe. Spika, makadirio ya makusanyo ya shilingi 171,687 milioni kutokana na vyanzo vya mapato ya ndani kwa mwaka 2010/11 ni sawa na asilimia 17.9 ya makadirio ya Pato la Taifa kwa mwaka 2010. Ikilinganishwa na mwaka 2009/10, kunajitokeza ongezeko la shilingi 25,518 milioni sawa na asilimia 17.5 kutoka shilingi 146,169 milioni zinazotarajiwa kukusanywa hadi kufikia mwisho wa mwaka unaoendelea wa fedha.

Kati ya mapato ya shilingi 171,687 milioni, mapato yanayotokana na kodi ni shilingi 160,976 milioni sawa na asilimia 93.8, wakati mapato yasio ya kodi yanatarajiwa kufikia shilingi 10,711 milioni sawa na asilimia 6.2 ya mapato yote. Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) inatarajiwa kukusanya jumla ya shilingi 91,735 milioni na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) inatarajiwa kukusanya shilingi 69,240 milioni.

Mapato ya Nje

Mhe. Spika, kati ya shilingi 266,950 milioni zinazotarajiwa kutokana na Washirika wa Maendeleo kwa mwaka 2010/11, misaada ya kibajeti ya asilimia 4.5 imetarajiwa kufikia shilingi 55,236 milioni. Kati yake, shilingi 37,593 milioni sawa na asilimia 68.1 ni ruzuku na shilingi 17,643 milioni sawa na asilimia 31.9 ni mikopo. Kama nilivyoeleza awali, fedha kwa ajili ya utekelezaji wa program na miradi ya maendeleo zinatarajiwa kufikia shilingi 211,714 milioni, sawa na asilimia 47.6 ya mapato yote.

Kwa kuzingatia mapato kutokana na vianzio vya ndani na yale ya misaada ya kibajeti, kunajitokeza nakisi ya shilingi 6,000 milioni katika bajeti. Serikali haikusudii kuongeza kodi kwa mwaka 2010/11. Badala yake, nakisi hiyo ya bajeti inatarajiwa kuzibwa kutokana na mikopo ya ndani kupitia hati fungate *(Makofi)*.

Mhe. Spika, pamoja na matarajio ya hapo juu, taarifa za karibuni zinaonesha kuwa Washirika wa Maendeleo wanakusudia kupunguza msaada wa kibajeti kwa Tanzania kutokana na sababu mbali mbali. Athari za kutekelezwa kwa hatua hiyo ni kupungua kwa misaada ya kibajeti kwa Zanzibar kwa karibu shilingi 18,000 milioni. Serikali imeshajiandaa na hatua za kukabiliana na hali hiyo *(Makofi)*.

MATUMIZI

Mgawanyo wa Matumizi

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/11 serikali inatarajia kutumia jumla ya shilingi 444,637 milioni. Kama nilivyoeleza katika Mpango wa Maendeleo, shilingi 251,204 milioni zinakadiriwa kutumika kwa shughuli za maendeleo kwa mwaka 2010/11, ambapo shilingi 211,714 milioni ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na shilingi 39,490 milioni ni kutokana na fedha za ndani.

Matumizi ya kazi za kawaida, ikiwemo mishahara pamoja na matumizi mengineyo, yanatarajiwa kufikia shilingi 193,433 milioni. Kati ya fedha hizo, shilingi 82,459 milioni ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 26,178 milioni ni matumizi ya ruzuku kwa taasisi mbali mbali na shilingi 84,796 milioni ni kwa matumizi mengineyo.

MFUMO WA BAJETI YA MWAKA 2010/2011

HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO

Mhe. Spika, pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya matumizi ya serikali, katika mwaka wa fedha 2010/11, serikali haikusudii kupandisha kodi yoyote. Badala yake, mkazo zaidi utawekwa katika kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato kutokana na vianzio vilivyopo.

Lengo ni kuona kuwa kabla ya kuongeza kodi, juhudi zinachukuliwa kwanza katika kuongeza ufanisi wa ukusanyaji na uwajibikaji wa ulipaji kwenye vianzio vilivyopo. Miongoni mwa maeneo yatakayoangaliwa ni uimarishaji zaidi wa usimamizi wa mapato yasio ya kodi na ufuatiliaji wa matumizi ya misamaha ya kodi. Lengo ni kuhakikisha kuwa misamaha inayotolewa inatumika kwa dhamira iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, ili kusaidia zaidi wakulima wetu kupata pembejeo na huduma za kilimo kwa gharama nafuu kwa kuharakisha mageuzi ya kilimo nchini na kushajiisha sekta binafsi kushiriki zaidi katika mageuzi hayo. Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/11, inapendekeza kutoa vivutio maalum kwa uwekezaji katika Sekta ya Kilimo. Vivutio vinavyopendekezwa kutolewa ni hivi vifuatavyo:-

a) Nafuu ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(Special Relief)* kwa ununuzi wa vifaa na usambazaji wa huduma za kuimarisha miundo mbinu ya umwagiliaji, kama vile huduma na vifaa vya ujenzi wa

misingi, barabara, bohari na maghala ya kuhifadhia nafaka na chakula kwa wawekezaji na Vikundi vya Ushirika vya Kilimo vilivyosajiliwa;

Aidha msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(Exemption)* utatolewa kwa zana za kilimo, kama vile mashine za kuvunia na kupurura nafaka, mashine za kukausha na kukata majani mahsusi zitakazotumika katika uendelezaji wa kilimo; na

b) Kusamehe Kodi ya *VAT (Exemption)* kwenye vifaa vitakavyotumika katika ujenzi wa mabanda au mahema *(green houses)* ya kuatika, kulelea na kukuza miche ya mimea, viungo, matunda na mboga mboga.

Hatua hiyo inalenga kupunguza gharama kubwa za ujenzi wa mabanda na mahema ya kuatika mbegu, kulelea miche na mimea kwa kuwapa nafuu ya kodi ya *VAT* wakulima kwenye ununuzi wa vifaa na huduma vitakavyotumika katika ujenzi huo.

c) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani *(Exemption)* kwenye uzalishaji wa ndani, usambazaji na uuzaji wa chakula cha mifugo ili kupunguza gharama za ufugaji nchini.

Mhe. Spika, ni jukumu la Sekta Binafsi kutumia fursa hii na kuimarisha huduma kwa wakulima, ili kuongeza uzalishaji na kunufaika na soko la ndani, na lile la nje. Utafiti wa hivi karibuni umeonesha kuwa bado kuna fursa ya soko kwa matunda, mboga mboga na bidhaa za mifugo katika sekta ya utalii.

MFUMO WA BAJETI KWA MWAKA 2010/2011

MAELEZO	Makadirio 2009/2010	Makadirio 2010/2011	Asilimia ya ongezeko
MAPATO			
A.MAPATO YA NDANI	**159,697**	**171,687**	**7.51**
i) Mapato ya Kodi	*148,932*	*160,976*	*8.09*
ii)Mapato yasiyo ya kodi	*10,765*	*10,711*	*-0.5*
B.MISAADA YA KIBAJETI	**50,214**	**55,236**	**10**
i) 4.5% misaada ya kibajeti	*50,214*	*55,236*	*10*
C.HATI FUNGATE (T/BILLS)	**3,506**	**6,000**	**71.14**
D.RUZUKU/MIKOPO YA NJE	**199,188**	**211,714**	**6.29**
i) Ruzuku ya miradi/programu	*96,879*	*79,022*	*-18.54*
ii)Mikopo ya miradi/programu	*102,309*	*132,792*	*29.8*
JUMLA YA MAPATO	**412,605**	**444,637**	**7.76**
MATUMIZI			
E.MATUMIZI YA KAWAIDA	**172,692**	**193,433**	**12.01**
i) Mishahara (Mawizara)	*73,763*	*82,459*	*11.79*
ii)Mishahara ya Taasisi (wanafaa)	*9,094*	*12,314*	*35.41*
iii) Matumizi mengineyo (Mawizara)	*38,942*	*39,796*	*2.19*
iv) Matumizi mengineyo (wanafaa)	*12,073*	*13,864*	*14.83*
v)Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS)	*38,820*	*45,000*	*15.92*
F.MATUMIZI YA MAENDELEO	**239,913**	**251,204**	**4.71**
i) Mchango wa Serikali	*40,725*	*39,490*	*-3.03*
ii)Mchango wa Washirika wa Maendeleo	*199,188*	*211,714*	*6.29*
JUMLA YA MATUMIZI	**412,605**	**444,637**	**7.76**

Chanzo: Idara ya Kukuza Uchumi na Bajeti, Wizara ya Fedha na Uchumi

Washirika wa Maendeleo

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru pamoja na kuwapongeza kwa dhati Washirika wetu wa Maendeleo kwa ushiriki wao katika kuisaidia Bajeti yetu.

Washirika hao wa Maendeleo ni pamoja na *BADEA*, BELGIUM, *UNDP*, *UNFPA*, UNICEF, *MCC*, *MCA*-T, CARE AUSTRIA, *DFID*, *WHO*, *JSDF*, *WSPA*, *WB*, *SIDA*, *IPEC*, EGYPT, JAPAN, *IDB*, FINLAND, *AfDB*, *GEF*, *GAVI*, *ILO*, *OPEC*, *USAID*, *GLOBAL FUND*, *DANIDA*, *CIDA*, *NORAD*, *KOICA*, SWEDEN, NORWAY, CHINA, *FAO*, *UNESCO*, *UNAIDS*, OMAN, JUMUIYA YA *AL-YOUSEIF*, *AFRICA CAPACITY BUILDING FOUNDATION*, REPUBLIC OF KOREA, *IAEA*, *UNIDO*, *EU*, USA, *JICA*, GERMAN, IRELAND, INDIA, HOLLAND, *IMF*, *IFAD*, CUBA, IRAN, *SSI*, *UN HABITAT* na United Kingdom *(Makofi)*.

Mhe. Spika, wakati serikali inaendelea na wajibu wake wa kutekeleza mageuzi ya msingi ya fedha na uchumi, mageuzi ya utumishi wa umma na utawala bora, ambayo ndio kiini cha kufikia malengo ya kukuza uchumi na kupunguza umasikini na hatimae tuweze kufikia malengo ya Milenia ifikapo mwaka 2015.

Napenda kuchukua fursa hii kuzidi kuwawakumbusha na kuwaomba Washirika wa Maendeleo kuendelea kutimiza wajibu wao wa kutusaidia, pamoja na kuongeza misaada ya maendeleo kama tulivyokubaliana katika Azimio la Monterey.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kueleza, changamoto kubwa za nje zilizojitokeza katika kipindi cha miaka kumi iliyopita ni kuzorota kwa uchumi wa dunia, kulikotokana na kuzuka kwa misukosuko ya kiusalama, kiuchumi, kifedha, mwenendo usiotabirika wa bei za mafuta, mabadiliko ya hali ya hewa na maradhi ambukizi duniani.

Misukosuko hiyo imesababisha upungufu wa chakula, mfumko wa bei na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi duniani. Athari za misukosuko hiyo zilienea kuanzia nchi zilizoendelea hususan zenye mlahaka mkubwa wa kifedha na kibiashara hadi nchi zinazoendelea, ikiwemo Zanzibar.

Mbali ya misukosuko hiyo ya nje, tumeshuhudia kuwa Zanzibar pia ilikabiliwa na misukosuko ya ndani, ikiwemo ya kuzimika umeme mara

mbili, matatizo ya wadudu waharibifu na maradhi kwenye mazao ambayo yaliathiri hali ya maisha ya watu kwa jumla.

Mhe. Spika, ingawa Zanzibar ilijinusuru sana na athari za misukosuko hiyo, bado taathira zake zinaonekana japo kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na nchi nyengine duniani. Serikali ilielekeza nguvu zake katika kuimarisha miundombinu ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na miundombinu ya utalii, kilimo na biashara. Halikadhalika, uimarishaji wa huduma za kijamii nao ulipewa kipaumbele hasa katika huduma za elimu, udhibiti wa malaria, UKIMWI na uimarishaji wa huduma za afya ya mama na watoto.

Kwa kutambua makali ya maisha kwa wananchi wake, serikali ilifanya mapitio na kuongeza kima cha chini cha mshahara kwa mwezi kutoka shilingi 25,000 kwa mwaka 2000 na kufikia shilingi 100,000 kwa mwezi mwaka 2010. Inatarajiwa kwamba maslahi ya wafanyakazi yatashughulikiwa vizuri zaidi baada ya kukamilika mapitio ya muundo wa watumishi (*scheme of service*) kwa kada zake zote.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema, kima cha chini cha mshahara wa wafanyakazi wa serikali kiliongezwa kama ilivyoahidiwa katika bajeti ya mwaka 2009/2010. Ahadi hii ilitekelezwa na serikali kwa awamu mbili kama ilivyoahidiwa awali. Kwa wakati ule haikuyumkinika kufanya mapitio kwa kima cha chini cha pencheni, ambacho nacho kimeendelea kuathiriwa na mambo mbali mbali ikiwemo mfumko wa bei.

Kwa mwaka ujao wa fedha, serikali inapendekeza kupandishwa kima cha chini cha pencheni kwa asilimia 67 kutoka shilingi 15,000 za sasa hadi kufikia shilingi 25,000. Serikali inaelewa kwamba bado kiwango kinachopendekezwa ni kidogo kulinganisha na hali halisi ya maisha. Hivyo serikali itaendelea kukifanyia marekebisho kiwango hicho kila hali inaporuhusu.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kazi kubwa na nzito ya kutayarisha na hatimaye kuniwezesha kuwasilisha mapendekezo haya ya bajeti mbele ya Baraza lako tukufu kwa wakati.

Shukrani zangu mahsusi nazielekeza kwa Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Makamishna, Wakurugenzi, Afisa Mdhamini Wizara ya Fedha na Uchumi Pemba pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi hasa watendaji wa Idara ya Ukuzaji Uchumi na Bajeti, kwa mashirikiano na mshikamano wao mzuri hadi kukamilisha zoezi hili la mchakato wa Bajeti ya Serikali *(Makofi)*.

Bajeti hii isingekamilika bila ya mchango wa watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa Wizara na Idara za Serikali; nao nawapa shukrani zangu za dhati *(Makofi)*.

Mwaka huu tumeendelea kupata mashirikiano mazuri kutoka taasisi zisizo za kiserikali ikiwemo sekta binafsi. Napenda kutoa shukrani maalum kwa ushiriki wao huo kupitia vikao vya matayarisho ya MKUZA II, Baraza la Biashara la Zanzibar, Mijadala ya Kiuchumi na Vikundi Kazi vya Mikakati ya Uimarishaji Mapato pamoja na mikutano mbali mbali ya utaratibu wa misaada. Moyo huu wa mashirikiano umerahisisha sana kukamilisha mchakato huu wa bajeti kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, kazi kubwa iliyotukabili na inayohitaji uwajibikaji na mashirikiano makubwa zaidi hasa baina ya sekta binafsi na sekta ya umma ni utekelezaji wa bajeti. Ni muhimu sana watendaji na wananchi wote kwa pamoja kuzidisha moyo na ari ya maendeleo. Kila mmoja wetu ana jukumu la kutimiza basi na tutimize wajibu wetu.

Mhe. Spika, kwa heshima, taadhima na unyenyekevu naomba sasa Baraza lako tukufu lipokee, lijadili na hatimaye lipitishe mapendekezo juu ya Mwelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2010/2011, ili yawe muongozo wa utekelezaji wa shughuli za serikali kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, serikali inapendekeza mbele ya Baraza lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kukusanya jumla ya shilingi 444,637 milioni pamoja na matumizi ya shilingi 193,433 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 251,204 milioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imeungwa mkono. Naomba nikiri kwamba hotuba hii ya bajeti ilikuwa ni refu kidogo. Kwa hivyo, nakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa ustahamilivu wenu kumsikiliza Mhe. Waziri, pia nawashukuru sana tuliowaalika kuja kuhudhuria kwenye kikao hiki ambao na wao wamekuwa watulivu kwa muda wote *(Makofi)*.

Kwa kuwa muda ni mfupi sana, basi naomba niwashukuru wageni wetu wote ambao wamehudhuria hapa na kuwa wasikivu, pamoja na kutulia kabisa katika kuona kwamba bajeti hii ya serikali inasomwa na kupitishwa hapa.

Kwa mujibu wa utaratibu majadiliano ya bajeti hii hayatoweza kujadiliwa leo kutokana na kifungu cha 93 (5) cha Kanuni zetu za Baraza. Hivyo kuna haja ya Mhe. Waziri atoe hoja kwa ajili ya kuahirisha mjadala huu kwa muda wa siku mbili.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kutoa hoja kwa Baraza lako liahirishwe hadi siku ya Jumatatu tarehe 14/06/2010 saa 3:00 asubuhi.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanakubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi)*.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda huu unatolewa kwa sababu ya vitabu hivi kwa ajili kwenda kupanga mipango yetu vizuri, ili siku ya Jumatatu tarehe 14 tuweze kuja kuchangia bajeti hii vizuri.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha kikao hiki hapo nje tumetayarisha dhifa, kwa sababu tumekaa muda mkubwa pamoja na wageni wetu kwa ajili kusikiliza hotuba ya bajeti.

Kwa hivyo, mara baada ya kuahirisha kikao hiki basi nawaomba wote, yaani Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wageni wetu tukutane hapo nje kwenye viwanja vyetu kwa lengo la kubadilishana maneno, kutafuna tafuna pamoja na kunywa. Kwa hiyo, nakukaribisheni sana kwenye dhifa yetu hapo nje.

Baada ya hayo naahirisha kikao hiki hadi siku ya Jumatatu tarehe 14/06/2010 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 12:35 Baraza liliahirishwa hadi tarehe 14 Juni, 2010 saa 3:00 asubuhi)